# *MASWALI NA MAJIBU*

Mmoja alisema katika Agano la Kale, "Nalifurahi waliponiambia "Na tuende nyumbani kwa Bwana."

1 Na sasa, ni jioni yenye joto kweli kweli. Na kwenu wageni mlio pamoja nasi, mnaweza kuona mbona Indiana ni pagumu kuishi humu katika hili—hili bwawa. Nawaambieni, ni 93° hapo, 93° Kwa hivyo mwoana, unapoenda chini palipo na kipimo cha joto 120° kama ilivyo Louisiana na Arizona, unaweza kutambua ni nini basi, jinsi unavyoingia kabisa. Kama hiyo—hiyo ingekuwa hapa, tungeangamia, ingekuwa hivyo tu. Lakini ni vizuri kuwa hapa kwa huu wakati wa kuabudu.

2 Baada ya kurudi nyumbani asubuhi hii, najisikia vizuri, vizuri sana kuhusu . . . naamini kuwa wengi waliponywa asubuhi hii ambao—ambao hawatambui, labda, kwa wakati huu, bali watapona; kwa sababu Neno la Bwana lilikuwa la thamani asuhubi hii mioyoni mwetu.

3 Nilikuwa tu . . . Nilipoanza kuondoka, ilionekana kama—kuta hizi zilikuwa karibu zinapumua kwa—kama kupuliza kwa Roho Mtakatifu hivyo ndani humu. Nami nilikuwa na furaha tele kwake.

4 Nilikuwa nikisikia Ndugu Smith, rafiki yangu, akiomba dakika chache zilizopita, mchungaji wa Church of God, Anderson. Na Ndugu Smith ana kitini kidogo, sidhani sisi tunazitoa hapa kwenye Maskani. Kama ye yote wenu hana hicho kitini kidogo, kisome. Hicho ni kitini kidogo cha kusisimua; hakika ni Kweli ya Kimaandiko. Nilivipeleka vingi Chicago na mahali mbalimbali kuvisambasa, kwa sababu hakika ni kitini cha na cha ajabu. Nami naona viliandikwa toka kwa moyo ulio mwaminifu na umpendao Mungu. Hamna nia ya kujinufaisha kwa Ndugu Smith, Mkristo kabisa. Kwa hivyo tuna furaha kushirikiana usiku huu na watu wa namna hiyo.

5 Naamini naona rafiki yangu mzuri, Ndugu Borders hapa toka—toka kule California. Na yeye alikuwa—amenifanyia kazi kuu hivi majuzi—kwa ajili ya Bwana—juu katika ile—pale—kuanzisha mkutano wa San Jose pamoja. Natumai utatufanyia kazi bora kwenye mkutano unaokuja Ndugu Borders. Nami nampenda Ndugu Borders kwa sababu naona ndani yake roho mpole, mnyenyekevu. Nami—nadhani hiyo ni thamani kuu. Nadhani mtu aliye na roho ya namna hiyo yampasa kuwa na furaha sana.

6 Kunao wengine wengi ndani humu, ambao hata siwezi kuwaorodhesha. Naona Ndugu Collins nyuma kule, ndugu yetu, na kisha wahudumu wengine na rafiki yetu mzuri Ndugu Sothmann, jamaa yake, toka Saskatchewan Kaskazini. Nami

namjua Ndugu Evans hapa, bado sijamwona, bali naona jamaa yake, na—toka chini kule—kule Georgia. Na kunaye Ndugu Palmer pale na—toka chini Georgia, na—na Ndugu West, naamini, toka Albama au Georgia. Unatoka wapi Ndugu West? Ni. . . ni. . . Enhee, Huntsville. Ndiposa. . . Eh, tunafuraha tele kuwaona nyote humu.

7 Na sasa, Ndugu Lyle, nyuma pale, Wood, toka kule juu Indiana ya kaskazini, na wapendwa wake. Nami nadhani Ndugu Charlie hapo, mwenzangu wa zamani—mwindaji mwenzangu toka chini kule Kentucky (mwindaji kuchakulo bora sana was pili Kentucky, mwindaji wa pili aliye bora sana kwa kuwinda kuchakulo. Yeye atafanya nijutie hilo. Vema!) na mke wake na jamaa. Na kwenu nyote, salamu za Kikristo.

8 Ndugu mdogo hapa, siwezi kukumbuka jina lake—hapa, watu mbalimbali. Lakini nyote mwajua kuwa hakika nafurahia kuja kwenu usiku huu kuabudu pamoja nasi maskanini.

9 Na sasa, usiku huu ni usiku usio wa kawaida maskanini, kwa sababu ni usiku wa maswali na majibu. Na hiyo huwa kwa kawaida mara moja kila mwaka mmoja au miwili. Na kusudi la kufanya hilo, ni kuweka mawazoni kile kilicho mawazoni mwa watu, ili nijue tu maswali yao ni nini. Kumfanya kila mtu atume swali humu, ndiposa lijibiwe toka jukwaani.

10 Sasa, katika hili sikupata—nilidhani yangekuwa mengi mno, lakini nina maswali machache tu. Kwa hivyo hatutachukua muda mrefu kuyajibu. Nilikuwa nawaza yangejaa sinia nzima, lakini machache tu na rahisi tu. Lakini baadhi yao yanahusu mafundisho.

11 Na katika mafundisho haya yanipasa kujibu maswali ya watu bila kujua hao ni akina nani (kwa sababu wengi hawakuandika majina yao kwenye maswali); na hivyo basi, yanibidi nijibu kulingana na mafundisho tunayoshikilia hapa maskaninini. Na kwa kufanya hivyo. . . Na kama inatukia kwamba yanavuka mpaka kwa baadhi ya ndugu zetu wanaotutembelea au akina dada, hatungalitaka kufanya hivyo kwacho chote kile. Hatuamini mtu kubishania mambo madogo ya Kimaandiko. Twaamini Kristo alikufa kutuokoa sisi sote, nasi sote tumeokolewa kwa Damu Yake.

12 Lakini kama kanisa na kama wa—watu, kusanyiko, yatupasa kuwa na mafundisho tunayosimamia kusudi tuwe ka—kanisa. Na mafundisho haya tunayoshikilia, ni bora sana tujuavyo kwa Neno la Mungu, Kweli ya Mungu. Sasa, una haki kamilifu kuyatazama kwa njia nyingine ukipenda. Na kwa hivyo, kama ni. . .

13 Mtu fulani akiuliza swali hapa. . . Baadhi yake ni magumu kidogo. Nami nitajibu sasa vizuri nijuavyo.

14 Sasa, hivi ndivyo ninayojaribu kushughulikia swali. Swali. . . Kama—mtu aweza kuchukua Andiko moja na karibu

angelifanya liseme lo lote utakalo liseme. Lakini Maandiko, kila Andiko ni Kweli. Na ni kamili sana, hata Mungu asiye na kikomo aliyelinena Andiko lile, ni kamilifu sana hata halina mwisho. Kwa hivyo, litasafiri toka Mwanzo hadi Ufufuo, jambo lile lile.Halitatofautiana. Ndiposa, kama Biblia ni Neno lililotiwa pumzi na Mungu halitajitatanisha lenyewe mahali po pote. Litaenda moja kwa moja Maandikoni mwote.

15 Sasa, wakati mwingi . . . Kama nilivyokuwa mkali kidogo nilipohubiri kuhusu Samson na Delila na kanisa katika malimwengu, lakini sikusudii kuwa mkali, lakini nakusudia kuwa mwaminifu, mwaminifu tu kama nia ya—yangu ilivyo.

16 Sasa, katika Maandiko. Hayo yakiwa Neno lisilokosea la Mungu, naamini kuwa kuna kitu kimoja pekee kiwezacho kutafsiri Maandiko sahihi, hicho ni, Roho Mtakatifu. Naamini huyo ni . . . Na Roho Mtakatifu aliyeandika Maandiko, na kusema hayafasiriwi kama apendavyo mtu fulani . . . Hivyo basi, kama yataelekea yote katika Maandiko, lazima awe Roho Mtakatifu yule yule basi, kote kote, kuyafasiri.

17 Lakini sasa watu wengi makanisani mwao na imani zao, wanatofautiana, kitu fulani kidogo anachokishikilia ambacho huenda kikawa kinyume chake kidogo. Kama ndivyo ilivyo, hebu fanya tu kama nifanyavyo ninapokula sambusa ya tunda. Sili mbegu. Ninapouma mbegu, naitupa mbegu na kuendelea kula sambusa yenyewe. Kwa hivyo ndivyo ikupasavyo.

18 Namwona Dada wetu Wooten ana mtoto mchanga anayasimama pale. Kama anasikia joto, Dada, na huna kiti, nashangaa kama mmoja wa ndugu zetu angechukua kiti toka ndani na kukiweka karibu na pepeo pale ili Dada aweza kupata mahali baridi pa kuketi. Tutafurahia kufanya hilo, nina hakika, ye yote wa ndugu hawa . . . Pepeo pale nyuma, Dada, vema— linapepea upande huu na kuna kiti. Kama unataka kukitumia, fanya hivyo tu.

19 Sasa, ye yote kati yenu ndugu anayetaka kuvua kote lake, fanya hivyo, jifanye ujisikie vema na mwenye furaha.

20 Sasa, nitaliuliza kundi hili, kama wataniombea mimi. Hili juma lijalo yanipasa kuenda California, kote kule, kwa ibada ya usiku mmoja. Usiku mmoja tu kuhubiri kwa Mkutano wa Kimataifa Wa Wafanyi Biashara Wakristo. Lakini wameutangaza na tunatarajia maelfu ya watu kuwa pale. Nami singetaka kuwaudhi. Nami niliwaambia ningekuja kama singekuwa Australia wakati huu, ambako nilikusudiwa kuweko. Kwa hivyo tuombeeni.

21 Na wengi wenu wasafiri wapendwa wa duniani humu mlio likizoni za kazi zenu za kila siku na mngependa kuwa katika mojawapo wa mikutano hiyo, kutakuwa na ibada ya siku tatu kule Cleveland, Tennessee, Church of God. Nadhani hilo ni Church of God la Kipentekoste, Mwenendo wa Tomlison.

Ndugu Littlefield, David Littlefield, ndiye mchungaji, Mkristo muungwana mzuri sana, Yeye ni Mwamerika toka Kaskazini, toka Bangor, Maine, lakini Mkristo halisi, ndugu mzuri.

22 Na kwa hivyo, ukiwa uko safarini na ungependa kuja, labda Jumatatu usiku itakuwa kubariki maskani makubwa mno waliyojengwa. Ndiposa, usiku wa Jumanne na Jumatano juma lijalo, Bwana akipenda—si hili juma lijalo, juma linalofuata hilo—kutakuwa na ibada ya uponyaji, itakayokuwa tarehe 6, 7, na 8.

Sasa kabla hatujafungua Neno, ningependa kama tungeinamisha vichwa vyetu kwa dakika chache kwa maombi.

23 Bwana Mungu, Baba mpendwa wetu sote, uliyefufua tena Bwana Yesu katika wafu na umemtoa kwetu kwa umbo la Roho Mtakatifu. Baada ya kusulubiwa alikufa, akazikwa, akafufuka siku ya tatu, na kupaa utukufuni, ambako sasa ameketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu, huku yu hai siku zote kutuombea, Kuhani Mkuu awezaye kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu na ajua hata shomoro mdogo sana ambaye angeanguka barabarani, Yeye angewezaje kutojali uaminifu wa wana Wake wanaoketi usiku huu katika hili jengo lenye joto kusikia Neno. Nina hakika, Bwana Mungu, kama hata hatukuuliza, kuwa ungemwaga baraka Zako juu yao kwa ajili ya ushujaa wao wa kutekeleza wajibu wao usiku huu.

24 Kuna wageni humu, Bwana; twawaombea na makanisa yao. Kunao wahudumu wa Injili waliowekewa mikono—waliochaguliwa na Mungu—waliomo humu, wanaostahili sana kuyajibu maswali haya kuliko mimi. Nami naomba, Bwana Mungu, kuwa utaruhusu Roho Mtakatifu atujie sisi usiku huu na kutupa mambo yafaayo kusema, ambayo yangeleta furaha isiyotamkika na iliyojaa utukufu mioyoni mwetu tunapoketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, tukisoma kirefu Maandiko bila uduhuru, bila husuda ila kujua tu yale yaliyo Kweli na kuabudu Kweli. Tujalie Bwana.

25 Tungeomba umbariki Mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville, aliyesimama kishujaa kutekeleza wajibu wake mwaka baada ya mwaka katika hari na shari kuchunga na kulisha kondoo wa zizi wanaokutanika hapa. Naomba ya kuwa Roho Wako atakuwa juu yake, msaidie. Na wabariki wote wanaohusiana na maskani haya. Na hivi karibuni, Bwana, kama ni mapenzi Yako, tunatarajia maskanani makubwa ya kupendeza yatakayojengwa hapa pembeni ambapo tunaweza kuwa na shule, tupate kuwafundisha wahudumu vijana na kuwatuma kwenye pembe nne za dunia ili waishindanie imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.

26 Bwana, tunazeeka, mimi mwenyewe, na hivi karibuni yanipasa kuipokeza Biblia hii mkononi mwa mtu mwingine. Tusaidie, Bwana, katika juhudi hii. Jibu maswali yetu usiku

huu kwa Roho Mtakatifu, kwa kuwa tunamtumaini, kwa maana twaomba katika Jina la Yesu Mwana Wako. Amina.

27 Sasa, najua kuna joto jingi sana, lakini sipendi kuruka swali hata nijue nimefanya haki mbele za Mungu kulijibu. Sasa, hatuna mengi sana; sikuyahesabu, ni machache sa—sana. Lakini huenda ikawa hatutayamaliza yote, lakini tunataka kufanya hivyo ikiwezekana. Nitamuuliza huyu msichana mdogo anayeketi hapa anayevalia nguo za rangi nyekundu-nyeupe... Njoo hapa, Mpendwa. Naamini huyo ni mshicha mdogo wa Ndugu Beeler. Nataka uyachukue maswali haya chini pale na kuyachanganya, mwajua ninalomaanisha, kuyapitanisha tu moja juu ya lingine, hivi, mwajua, ili—kisha unirudishie. Ona? Ili nisichanganyishe maswali ya mtu ye yote mwajua, nikidhani nilijibu moja, na sikufikia lingine; singetaka hivyo. Hebu na msichana mdogo huyu ayachaganganishe pamoja, ndiposa tutayachukua yaliyo juu na kuyajibu tunapoendelea.

28 Sasa, kama kungekuwako (asante, mpendwa)—kama kungekuwako swali mawazoni mwa mtu fulani, nataka kusema ya kwamba ningefurahi kama baada ya kujibu swali lako na yaonekana haukuridhika, basi inua mikono yako na kujibu. Kwa maana mimi pia ninayo hapa kamusi ya Kiyunani, Kiebrania—kamusi ya maneno asili ya Kiyunani na Kiebrania pia, kwa maelezo ya maneno (mwaona?), kwa sababu wengine wao wanauliza maneno—ya Kiebrania na ya Kiyunani pia.

29 Na sasa, Bwana atusaidie tunapojibu. Na hebu nieleze dhahiri...(Je, mwaweza kunisikia vizuri kule nyuma, inueni mikono yenu kama mnaweza. Hilo ni zuri). Hebu nieleza dhahiri sasa, kuwa katika kujibu maswali haya si kwa udhuru wo wote, lakini kila mmoja akumbuke kuwa katika maskani ifikapo kwa mafundisho, yatubidi kujibu kulingana na msimamo wetu hapa, si kupinga mawazo yenu, lakini ku—kudhihirisha msimamo wetu. Na wakati mwingine tunayaeleza kwa mkazo sana. Kwa hivyo kumbuka, ni kuwahakikishia tu waabudu.

**75.** Sasa, la kwanza juu. Enhee, naam, hili ni swali ndogo. Si swali...Vema, ni swali. **Ni mtu ambaye anataka mahojiano ya kibinafsi pamoja nami juma la kwanza.**

30 Sasa, hayo mahojiano, nitakwambia jinsi tufanyavyo hayo. Ilikuwa kuchagua tu bila taratibu *ye yote yule, nani wa kwanza, huyu, yule,* lakini tuna utaratibu kwa hayo. Na hivyo basi kuna watu wengi wajao katika mistari ya kuombewa, ambao labda hupitia kwa mstari mwepesi, ama wana jambo wasilojua la kutenda, kisha, wao wanataka kusikia toka kwa Bwana. Sasa wana haki kamilifu kwake, hiyo ndiyo sababu hiki kipawa cha kinabii kilitolewa, kwa ajili hiyo, kusudi hilo pekee.

31 Katika Biblia kama walitaka kujua lo lote, walienda kwa manabii, nao waliomba na kuimba nyimbo hadi Mungu alipojibu. Naam, Yeye si Mungu ambaye angelisha kundi moja

na kuliua lingine kwa njaa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na kwa hivyo, hiyo ndiyo sababu Yake.

32 Kwenye haya mahojiano ya kibinafsi, tunapochukua kisa, sikiachi hadi nisikie toka kwa Mungu hivi ama vile. Inachukua muda. Kama tukichukua miezi sita au mwaka, tunakaa moja kwa moja nacho hadi tutakapopata BWANA ASEMA HIVI. Ona? Na hivyo basi, inachukua muda, na kuna maelfu wa—wanaopiga simu. Lakini sisi . . .

33 Hivi majuzi nilikuwa na mtu ndani mle kwa ile—naamini ilikuwa miezi baada ya miezi ambayo mtu huyu alikuwa ametafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, Mbatisti. Lakini hatukumwachilia, tulimruhusu tu aje, na mwishowe kwa neema ya Mungu kwenye mahojiano ya kibinafsi . . . Aliingia tu—yeye kila mara alitaka kuona ono nini shida—na ono lile likaja, naye akampokea Roho Mtakatifu akiketi papo hapo kitini mwake.

34 Kisha M—Mkatoliki, aliyeokoka hivi majuzi, akaja toka Chicago majuzi ambaye amekuwa kwenye mahojiano ya kibinafsi—akijaribu kuingia—kwa karibu miaka miwili; lakini kwenye mahojiano yake ya kwanza, dakika kumi na tano chumbani, Bwana akaonyesha ono, sababu na kadhalika, akafunua jambo lote, kile alichopaswa kufanya kabla hamjapokea Roho Mtakatifu. Ona, hiyo ndiyo kazi yake.

35 Sasa, kama mtu ye yote kwa wakati wo wote . . . Wakati simu inapokuja nao wanataka kuona au kuwa na mahojiano hayo, kama wakipiga simu, BUtler 2-1519, afisi inaweza kukuarifu lini hasa mahojiano hayo yaweza kuwepo. Ndiposa eleza mahojiano yako ni ya nini, ili wajue yatapewa muda gani. Basi hiyo huifanya ya haki, na kila mtu . . . Ndipo kama muda huo hautoshi, tunarudia kisa hicho tena. Inawekwa kwenye orodha, nasi tunaiweka hadi tusikie toka kwa Mungu kwa ono au njia fulani ambayo Mungu hunena. Kwa hivyo, hivyo ndivyo mahojiano yetu yafanywavyo.

36 Kwa hivyo, ona, ninapokuwa nje, watu hudhani wakati mwingine, "Ndugu Branham, huoni watu vya kutosha." Huwezi kuonana na watu na kuwa na Mungu wakati uo huo. Ona? Nina mtu mmoja mawazoni, nami—nami niko kwenye pango au kitu kingine nikiomba, na—na . . .

37 Nataka kuona hili lasema nini. [Ndugu Branham ajisomea mwenyewe kijikaratasi—Mh.] Enhee, naam. Naam, ilikuwa mtu huyu (Gene ndiyo kwanza aiweke hapa) kuwa . . . Mtu fulani alikuja toka Chicago majuzi, ambaye dakitari alitaka kuupasua moyo wake, na kuupasua aone ulikuwaje ndani. Na Roho Mtakatifu alifunua ilikuwa nini hasa, naye hakuhitaji kupasuliwa; aliponywa. Kwa hivyo waona, hilo lamaanisha mengi. Na kuonyesha jinsi inavyochukua muda, nilingoja mimi mwenyewe jibu toka kwa Mungu, ono, kwa miaka kumi na mitano. Mungu . . . Ndiposa mwingine aja na haimlazimu

kungoja kwa dakika tatu. Ona? Ina . . . Mungu hujibu kwa wakati Wake Mwenyewe. Hatuisimamii, inatusimamia sisi.

**76.** Sasa, swali la pili lililo juu ni . . . **Ndugu Bill, Je, Bwana anaweza kunitumia kutenda kazi inayofaa katika kusanyiko lisiloamini karama za roho?**

38 Hakuna jina kwalo, lakini mtu huyu ataka kujua kama Bwana aweza kumtumia kutenda kazi pamoja nao kwa kuwa wametawazwa katika kusanyiko zisizoamini karama za kiroho. Nashuku hilo sana.

39 Ninashuku sana, rafiki mpendwa, kuwa Bwana angefanya kazi kikamilifu kwako, kwa sababu wewe umeunganika na wasioamini, na Biblia ilisema, "Msijifunge nira na wasioamini, lakini tokeni kati yao, mkajitenge, asema Bwana, ndipo nitawapokea." Naamini kama unaishi mjini, ambapo mna kanisa linaloamini ishara na karama za kiroho na una vitu hivyo vikitenda kazi ndani yako, ningeenda kwa kanisa hilo ambamo wanaviamini.

40 Ndiposa naweza kusema jambo moja, kama vile nimefanya—kawaida—nataka kutoa Andiko. Wewe labda, rafiki mpendwa, umejaribu uwezavyo kujaribu kuwafanya watu hawa waamini, ulijaribu kuwafanya waamini, nao hawakufanya hivyo, labda. Basi nitakupa Andiko ambalo naamini kuwa Bwana Yesu angependezwa nasi kutoa.

41 Kama umejaribu, kama umenena na mchungaji, kama umeongea na watu mbalimbali nao wamelipuuza kabisa na hawaliamini, haya ndiyo Yesu aliyosema katika Mathayo 7:6 kuhusu mambo kama hayo.

> *Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe . . . lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, . . . wakageuka na kuwararua.*

42 Kwa hivyo siamini kuwa ningeshiriki na kusanyika ambalo haliamini Injili nzima ya Bwana Yesu Kristo, kuamini kuwa ni Yeye yule, jana, leo na hata milele. Niketipo katika kusanyiko na kumwona Yeye akitenda kazi na kufanya kama tu vile alivyosema angetenda, naamini ningejisikia tu kama—nina haki ya kuwaambia watu watoke kati ya mambo kama hayo na kujipatia ka—kanisa nzuri linalohubiri Maandiko yote na kuyaamini.

**77.** Sasa, swali linalofuata ni: **Ni kweli kuwa hujaokolewa isipokuwa umempokea Roho Mtakatifu?**

43 Ingechukua masaa matano kuzungumzia hayo. Unapomkubali Kristo kama Mwokozi wako na uko tayari kwa ubatizo katika maji, bado hujaongoka; umeamini tu *hata* ukatubu. *Kuokoka* maana yake, "kubadilishwa."

44 Sasa, kulifanya hili dhahiri kabisa, Yesu alimwambia Petro ambaye pia alikuwa amemfuata Yeye kwa miaka 3 1/2 . . . Na

katika Kitabu cha Mathayo sura ya 10 Yesu alimpa Petro nguvu dhidi ya pepo wachafu, aende na kuwatoa, kuponya wagonjwa na kuhubiri Injili. Yeye alikuwa na nguvu ya kufanya mambo haya. Na katika Yohana Mt. 17:17 Yesu alimtakasa Petro kwa hiyo Kweli, kasema Neno lilikuwa Kweli, na Yeye alikuwa Neno. Na pale—kabla ya Pentekoste Yeye alisema, "Nawe utakapookoka, basi waimarishe ndugu zako." Unachukua tu hatua kuendea wokofu unapoamini na kutenda.

45 Sasa, najua wengi wenu, marafiki zangu Wabatisti na Wapresbiteria, hamkubaliani na hilo, kwa sababu mnarudi kwenye Andiko hili...Sasa, hapa ndipo nasema yanibidi nilithibitishe zaidi. Ona? Mnarudi nyuma kwenye Andiko: Ibrahimu (Warumi 4) *alimwamini* Mungu, na *ikahesabiwa* kwake au *kuwekwa kwake* kuwa haki. Ibrahimu *alimwamini* Mungu, na Mungu akamhesabia haki juu ya msingi wa imani yake kuamini. Lakini kumthibitishia Ibrahimu, Yeye alimpa (alimwekea, kuwa dhambi zake hazikuhesabiwa, ndipo Yeye alikuwa alifutiliwa dhambi zake), kwa sababu huyo alikuwa ameamini, Yeye alimpa ishara. Na hapo ndipo ninyi, marafiki zangu wapendwa Wapresbiteria na Wabatisti, mnakosa kuliona. Ona? Yeye alimpa muhuri wa tohara kama ushuhuda, kama thibitisho, kuwa alikuwa amepokea imani yake katika Yeye. Na hiyo ndiyo sababu Paulo katika Matendo 19 aliwaambia hao ndugu Wabaptisti, ambao Apolo alikuwa mchungaji wao, wakiiamini Injili kama Yohana alivyoihubiri, "Je, mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Mwaona, walikuwa wameamini ila walikuwa bado hawajaokoka.

46 Sasa, tunachukua vibaya—katika neno *kuokoka* siku hizi. Tungesema kuwa mtu aliyeokoka ni mtu aliyeacha kunywa pombe na kila kitu na huenda kanisani, au akajiunga na kanisa. Yeye huenda akajiunga na kanisa, lakini hiyo si ishara kuwa ameokoka. Yeye hajaokoka hadi maisha yake ya kale yamekufa, na amezikwa katika Kristo, na amefufuka pamoja Naye katika ufufuo wa maisha mapya, wakati Roho Mtakatifu ameumba ndani yake tumaini lililo hai la Uzima wa Milele ambalo huja tu kwa Roho Mtakatifu. Ona?

47 Basi, sasa, najua hilo Andiko kuu, nililitumia mimi mwenyewe—nimeliandika hapa— Yohana Mt. sura ya 5, kifungu cha 24. Ni Andiko ninalopenda sana. Kwa kuwa Yesu alisema hili: "Amin, amin, nawaambia, 'Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa Milele." Hebu niisome, ili niipate kikamilifu kabisa. Yahana Mt. 6, nami nawatakeni msikize kwa makini tunapoyaingilia Maandiko haya, 5 na kifungu cha 24.

> *Amini, Amini, nawaambia, Yeye* ayasikiaye maneno yangu *na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.*

48 "Yeye aniaminiye Mimi." Sasa, Maandiko yasema kuwa hakuna mtu awezaye kusema Yesu ni Kristo ila tu kwa Roho Mtakatifu. Kwa hivyo huwezi kuamini kuwa Yesu ni Kristo isipokuwa umepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unashuhudia tu au unasema tu yale Maandiko yasemayo, unasema yale mchungaji asemayo, kusema asemayo mama, ama yale mhubiri fulani mzuri asemayo. Lakini hujui hilo wewe mwenyewe hadi Yeye ameshuhudia ufufuo Wake kwako. Na hakuna mtu awezaye kumwita Yesu Kristo ila kwa Roho Mtakatifu.

49 Kwa hivyo, swali ni, ya kwamba mtu ameokoka, naamini, kama yeye anatazama kuelekea Kalvari, na kufa katika hali hiyo. Bila shaka naamini yeye ataokoka; naamini yeye atapita kama yeye hajapata nafasi hapo mbeleni. Lakini inategemea... Unarejea kwa ule mwizi aliyekuwa akifa msalabani. Lakini kumbuka, hiyo ilikuwa nafasi yake ya kwanza na ya mwisho. Unayo moja usiku huu. Usingoje hadi wakati huo, kwa sababu huenda isewe hivyo kwako. Huenda usiwe na maungamo kitandani unapokufa. Nawaambieni, hayo ni sawa, lakini si nafasi nzuri ya kungojea. Usingoje hadi kitandani unapokufa; acha hiki kiwe kitanda chako cha kufia hivi sasa, upate kufa sasa na kuzaliwa mara ya pili na Roho Mtakatifu.

Sasa, kwa hili swali linalofuata...Sasa, kama kuna swali juu ya hilo inua tu mkono wako. Nitafurahi kufanya vizuri niwezavyo.

**78. Je, waweza kupata po pote ambapo mitume walipokea Ushirika baada ya Pentekoste? Je, Paulo alikusudia kuwa watu hawakupambanua Neno? Njia tu ya kuabudu Mungu ilikuwa kwa Roho Mtakatifu? Je, ukinywa divai na biskuti, magonjwa na kulala mauti hukupata?**

50 Sasa, hapa labda ni mahali ambapo naamini mtu huyo mpendwa aliyeuliza hili bila shaka ni mwaminifu kabisa katika hili, lile wanalouliza, au hawangeuliza. Nami—Ndugu yangu au Dada, ye yote yule, nalijibu tu kwa uaminifu na unyenyekevu kama ulivyolijibu—au ulivyouliza.

51 Nawatakeni mfunue pamoja nami Kitabu cha Matendo sura ya 2, pamoja na—tunaanzia kifungu cha 42. Sura ya 2 ya Matendo, nami nitaanzia, kama nilivyosema, kwa kifungu cha 42.

52 Sasa kumbuka, siamini kuwa naweza kusema tu hasa ambapo Maandiko husema kuwa Paulo alipokea Ushirika, na kisha Petro akaja na kuupokea; lakini wanaponena kuhusu kusanyiko, hilo lilikuwa kwa jumla, kila mtu. Nami siamini kuwa Paulo angehubiri jambo fulani na kuwaambia wengine wafanye, ambalo yeye hangefanya. Kwa hivyo katika Matendo twapata haya:

> *Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume... ushirika,...*(Tazama! Wakidumu, kanisa lote, huo

mwili) . . . wakawa wakidumu *katika fundisho la mitume, na katika ushirika, . . . (na,* kiunganisho pale. Ona!) *na katika kuumega mkate, . . .* (Hiyo ni Ushirika.) *na katika kusali.*

53 Mitume, waliokuwa wahubiri . . . Walidumu katika mafundisho yao, ya kuumega mkate (Ushirika), na katika ushirika, na katika kusali. Basi kama hilo linaondoa Ushirika kwa mitume, linakuondoa kusali pia kutoka kwa mitume. Ona? sasa, hebu tuendelee kusoma. Ona?

*Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume.*

*Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo,*

*Na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.*

*Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, . . .* (Hao ni mitume na wengineo) . . . *wakimega mkate* . . . (Ushirika kila wakati walipokutana) . . .

54 Hilo lilikuwa fundisho la mitume na la kanisa la kwanza, kuwa kila wakati walipokutanika walipokea Ushirika. Kila wakati! Sasa, najua ninyi Wakristo mwendao kwa Christian Church (kanisa la Campbellite, kama tunavyolijua, kama . . . kwa sababu kuna mawili, moja ni Church of Christ, na lingine ni kanisa la Campbellite.), mwasema, "Twaupokea kila Jumapili asubuhi. Tuna Andiko kwake." Mna Andiko nzuri sana kwalo kuliko Maskani ya Branham. Maskani ya Branham hupokea mara moja kwa mwezi. Lakini Andiko ni kila mkutanikapo. Naam. Hilo ni kila wakati.

*Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, . . . wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe,*

55 Ona, kila wakati mitume, walipokuwa na hivi vikundi vya maombi, mikutano hekaluni, nyumba kwa nyumba; kila walipokutana, walimega mkate, na kupokea Ushirika.

56 Sasa, Paulo, katika 1 Wakorintho tuta—tungesoma pia sura ya 11, ambapo twatumia hapa kwa Ushirika . . . Huenda nikapasome ili paweze kuwasaidieni, 1 Wakorintho sura ya 11. Msikie Paulo akinena sasa, kifungu cha 23.

*Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate,*

*Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.*

*Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, . . .* (kikombe sasa) *. . . Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi . . ., kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.*

*Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*

57 Ona? Ni ushirika. Natambua na nakubali kuwa mwi—mwili wa Bwana, Neno lililo hai, ni Kristo Mwenyewe. Lakini hii ni mifano kama tu Ubatizo, na Kutawadha Miguu, na maagizo mengine ya Kanisa. Lakini Ushirika ni muhimu hasa kwa mkate, sasa, mkate na divai.

*Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, . . .*

58 Sasa, swali liliulizwa hapa: "Je, ukipokea—ukinywa divai na biskuti, magonjwa na kulala mauti hukujilia?" Ona hilo . . . Naamini swali hilo ni, ya kwamba ibada iliyoko tu, ni katika Roho Mtakatifu, kuabudu katika Roho Mtakatifu. Hiyo ni Kweli hasa. Inakupasa kuabudu . . . Kuabudu kwote ni katika Roho Mtakatifu, na Paulo anajaribu kusema hapa, kuwa lazima uwe katika Roho Mtakatifu kabla hujatekeleza hili au unakula na kunywa hukumu juu yako mwenyewe (ona?) kabla hujatekeleza hili, kabla utaratibu haujafuatwa.

59 Sasa, kuunga hilo mkono, nina maandishi hapa ya Josephus, ambapo yeye alidai kuwa Wakristo wa kwanza baada ya kifo cha—cha Yesu, kuwa walidhaniwa kuwa wala watu, kwa sababu waliutwaa mwili wa Bwana na kuula. Nao walidhani walikuwa wameuchimbua, na kuuondoa, na walikuwa wakiukata vipande, na kuula. Nao walikuwa wakipokea Ushirika. Ona?

Sasa, tazama, mbona Andiko hili—jinsi Paulo asema hapa.

*Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, . . .*

60 Aule mkate. Sasa, najua Yesu ni Mkate wa Uzima; hilo ni kweli. Lakini huu ni mfano kama tu wa ubatizo. Ubatizo haukuokoi; ubatizo ni ishara tu kuwa wewe unashuhudia kwa kusanyiko kuwa unaamini katika kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo. Haukuokoi. Maji hayatakuokoa. Ni imani yako ikuokoayo. Lakini ubatizo ni amri, na lazima utekelezwe, kwa sababu Mungu hawezi kusema mbatizwe, ndiposa ageuke na kusema haina haja kutekelezwa. Yeye hawezi kutoa kupokea Ushirika, na ageuke, na kusema hakuna haja ya kuupokea. Huna budi kuupokea. Ni amri ya milele ya Mungu.

*Maana alaye na kunywa, hula kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.*

61 Sasa, mwaona pale? Inakurejeza kwa Mkristo anayejaribu kupokea Ushirika ambaye hayuko katika Kristo, asiyeshiriki

katika Roho; yeye hastahili kuupokea. Naye apokeapo Ushirika huu, yeye anakula na kunywa hukumu kwa nafsi yake, kama yeye anatoka akivuta sigara, akidanganya, akiiba, akifanya uasherati, au kitu kama hicho, au kutokuishi maisha ya Kikristo. Na watu wanaona maisha anayoishi, ndiposa anaingia, anachukua agizo hili la mauti na—na mwili wa Kristo akichukua ndani yake mfano kuwa—kuwa yeye amepokea Kristo Neno katika moyo wake na akichukua mfano huu ndani mle nyuma yake, Yeye alisema anakula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili wa Bwana.

62 Sasa, katika dakika chache nitafikia swali lilo hilo, tukilifikia, kwa sababu ni jambo la namna ile ile ya kumkufuru Roho Mtakatifu. Ona? Kwa sababu unakiri kitu fulani, na kuwa mnafiki, ambapo yakubidi usifanye hivyo. Vema! Hebu nimalize hili, ona, ndiposa tutakoma.

> *Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wamelala.*
>
> *Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa.*
>
> *Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu pamoja na dunia.*
>
> *Kwa hivyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojane.* (Sasa, tazama).
>
> *Mtu akila—mtu akiwa na njaa, . . .*

63 Usiingie. . .kwa sababu kwa Andiko lingine hapa, wao walikuwa wakileta vyakula, na vinywaji vingi, na vitu kama hivyo, hadi walikuwa wakiifanya nyumba ya Bwana kama tu ma—mahali pa—pa karamu, na kulewa mezani pa Bwana. Mwakumbuka hayo katika Kitabu cha Wakorintho hapa. Walilewa mezani pa Bwana. Lakini Paulo alisema hapa:

> *. . .mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake; msipate kukutanika kwa hukumu. Na hayo yaliyosalia nijapo nitayatengeneza.* (Ona?)

64 Kwa hivyo basi, naamini kuwa kula biskuti . . . Sasa, siamini kuwa ule mkate usiotiwa chachu wapaswa kubadilishwa na biskuti. Naamini kuwa lazima uwe mkate mtakatifu usiotiwa chachu, namna ya mkate usiotiwa chachu uliookwa Misri. Nami naamini kuwa Damu haipaswi kuwa maji ya zabibu, inapaswa kuwa divai. Maji ya zabibu huwa machungu, na huharibika yanapokaa sana. Lakini divai huwa bora na yenye nguvu inapokaa sana; haipotezi nguvu zake kamwe. Na Damu ya Kristo haiwi chungu na kuharibika; inapokaa sana, inakuwa na nguvu zaidi na bora zaidi siku zinapoendelea kwa mwamini. Na ni divai halisi na mkate pia. Mkate wa ushirika lazima uokwe na watu ambao wamejitolea na kujitakasa kwa Mungu.

65 Nilihudhuria kanisa fulani siku moja ambapo waliuchukua maskini mkate huu wa kawaida ambapo wenye dhambi wanalaani na kutenda yasiyofaa, na kuukata maskini mkate huo na kuubandika pale na kunywa maji ya machungwa. Kwangu hilo ilikuwa—ilikuwa kudhihaki. Naamini yapasa iwe hasa jinsi Maandiko yalisema inapaswa kuwa bila kutofautiana hata kidogo na Maandiko, kaa kwayo.

**79.** Swali. Sasa! **Ndugu Branham, ni kweli kuwa Shetani wakati mmoja alikuwa Mbinguni na akatupwa nje, yeye na malaika zake wakashuka duniani, au ilikuwa ni ono kama Yohana alivyoona kwenye kile Kisiwa cha Patmo? Nauliza hili kwa sababu hii, kwamba, niliambiwa ilikuwa ni ono.**

66 Yohana aliiona kama ono, lakini ilikuwa ikitendeka vivyo hivyo. Kama mtafungua Isaya 14:12. Sasa, haya yanaenda pole pole, lakini kwangu, ni—ni mafunzo. Na ni kitu ambacho... Labda mwadhani, "Vema, sina haja ya hilo sasa." Hujui tu jinsi huyo Roho Mtakatifu anavyolishwa Neno la Mungu. Hana budi kupata Neno apate ku—kulila, kwa sababu Roho Mtakatifu hula tu, Neno la Mungu pekee. Mwamini hilo? Biblia ilisema hivyo. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu." Vema! Sura ya 14 ya Isaya, nami naamini hapa sasa tutaanzia kifungu cha 12. Hebu tusome sasa kuhusu yule Nyota ya Alfajiri.

> *Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri,*...(kuanguka toka Mbinguni)...*mwana wa asubuhi!*...(Kiumbe cha kimalaika toka Mbinguni.)
>
> *Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe* uliyetembea—uliyeangusha *mataifa!*
>
> *Nawe ulisema moyo mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kaskazini.*
>
> *Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu.*

67 Kwa hivyo waona halikuwa ono. Bila shaka, Nyota ya Alfajiri alitupwa toka Mbinguni.

68 Sasa, hebu tufungue Agano Jipya katika Luka 10:18, kwa dakika moja hivi, na kuona yale Yesu alisema. Katika Kitabu cha Luka, na Biblia zenu sasa, huko ni kujaribu kufikia maswali haya, Luka 10:18:

> *Akawaambia,*...(Yesu akinena)...*Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme.*

69 Ona, Shetani alikuwa yule malaika mkuu wa kwanza wa Mungu. Wakati mmoja Yeye alikaa Mbinguni. Wakati mmoja alikuwa mtu mkuu sana kuliko wote mbinguni mbali na Mungu.

Yeye alikuwa msaidizi mkubwa wa Mungu kwa ushirika, naye akawa mwenye kiburi moyoni mwake.

70 Na si hivyo ndivyo watu wanavyokuwa siku hizi? Hebu Mungu ambariki mtu na aweke tumaini ndogo ndani yake, naye awa anayejua yote. Yeye huwa . . . Yeye yambidi aanzishe dhehebu, au yeye afanye kitu fulani tofauti. "Mbona umeanguka kutoka Mbinguni, Ewe Nyota ya Alfajiri!"

71 Ni . . . Mungu ana wakati mgumu kujaribu kumpata mtu fulani ambaye Yeye aweza kumshughulikia, atakayedumu mnyenyekevu, na mpole, na akae mahali pale hadi Mungu amwite akafanye kitu fulani (mwaamini hilo? Ona?), mtu ambaye Mungu aweza kumbariki naye bado atadumu mwenyewe mtu, si kuwa malaika wala Mungu. Mara tu mtu abarikiwapo na ana kitu fulani kidogo alichopewa, yeye ataka kuwa mungu; yeye ataka kuwa ma—malaika. Yeye ataka kuwa mtu mkuu. "Kile nifanyacho, kile . . . Mimi na mimi na vyangu . . ." hayo yote. Hiyo ni nia mbaya. Mungu anamtafuta mtu ambaye Yeye angembariki na kumumwagia baraka, na—na jinsi anavyombariki ndivyo mtu huyo anavyozidi kuwa mdogo.

72 Na hutapata zaidi ya Mungu hadi uwe si kitu. Yakubidi ujifanye mwenyewe mdogo. Yeye ajikwezaye, Mungu atamdhili. Yeye ajidhiliye, Mungu atamkweza. Huna budi kuwa mdogo kabla hujawa mkubwa. Na hutakuwa kamwe mkubwa kwa nafsi yako; utakuwa tu mkubwa kadiri Mungu atakavyokuwa mkubwa ndani yako. Ona?

73 Kwa hivyo yule Nyota ya Alfajiri yuko duniani leo akijaribu kufanya kazi kanisani kutimiliza kusudi lile lile aliloanzisha kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yule Nyota ya Alfajiri alifukuzwa Mbinguni. Vema.

74 Naamini kuna jambo moja hapa, Ezekieli sura ya 28, kifungu cha 12. Hebu tuone kile hilo lasema katika Ezekieli 28:12. Nami nina hakika kuwa kwa kusoma kirefu haya, na kuyachunguza, kuona kile BWANA ASEMA HIVI, ndipo tutajua kama yeye kweli alianguka kutoka Mbinguni au ilikuwa tu ono-28 na 12. Vema. Naamini hicho ndicho nimeandika, 28:12. Basi tuanze.

Sasa, hili ni jambo kuu hapa: laiti tungelikuwa tu na wakati wa kuendelea kuhubiri kidogo (ona?), maana ni jambo muhimu sana.

75 Sasa, kama nilivyoanza tu kuweka msingi hili, kuwa huyo Nyota ya Alfajiri Mbinguni alijaribu kujikweza mwenyewe na hata awe juu kidogo kuliko Bwana wake. Naye akamsaliti Mikaeli, na kujifanyia mwenyewe ufalme mkuu kaskazini, akashuka chini. Sasa, pia yeye na malaika zake wakafukuzwa.

Mtu huyu aliuliza kuhusu Ufunuo . . . Hiyo ni Ufunuo 12, kwenye Kisiwa cha Patmo.

Lakini sasa tazama hili hapa, kwenye kifungu cha 12, na tazama jinsi yeye anavyoketi katika ufalme wa mwanadamu.

76 Watu wangapi hapa wanafahamu kuwa shetani huongoza kila taifa chini ya Mbingu? Shetani anaongoza Marekani. Shetani ndiye serikali ya Marekani. Shetani ndiye serikali ya Ujerumani. Yeye ni serikali ya kila taifa chini ya mbingu. Shetani huongoza kila taifa, Biblia yasema yeye afanya hivyo. Soma Mathayo sura ya 4. Shetani alipomchukua Yesu juu ya ule mlima, na kumwonyesha falme za duniani, na kudai kuwa ni zake, na kusema, "Nitakupa ukiniabudu," Yesu hakusema kamwe, "Umedanganya, Shetani." Yeye alijua zilikuwa zake. Lakini pale katika kile Kitabu cha Ufunuo, kasema, "Furahini, ninyi mbingu na nchi, kwa maama uflame wa dunia hii umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na Kristo Wake. Naye atamiliki duniani."

77 Yesu alijua ya kuwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu serikali zote na falme zote zitavunjwa, na Yeye atakuwa Mungu na Mtawala juu yao wote. Yeye alijua atarithi hizo zote, kwa hivyo basi, Yeye alimwambia Shetani, "Rudi nyuma Yangu, Shetani!" kwa kuwa Yeye alijua yale ilimbidi kufanya.

Sasa, sikiza hili, Roho wa Bwana juu ya nabii huyu Ezekieli, akinena, si kwa huyu mfalme, lakini kwa yule roho katika huyo mfalme. Tazama hili sasa.

78 Mwakumbuka asubuhi hii nilipowaonyesheni ninyi jinsi katika Maandiko kanisa liliingia kwenye njia mbovu kwa kuchukua taratibu za wanadamu. Vivyo hivyo, Israeli iliacha njia kwa kumkataa Mungu kama Mfalme wao na kumtaka Sauli kuwa mfalme. Na Mfalme wao halisi, Yesu, alipokuja, hawakumjua Yeye kwa sababu mahubiri Yake—Yake na mafundisho Yake yalikuwa tofauti sana na ya wafalme wa duniani, hata hawakumjua Yeye. Na leo, wakati Mfalme wa Kanisa, Roho Mtakatifu, awapo hapa, na Yeye aingiapo Kanisani kuwafanya watu wazaliwe mara ya pili, kuwapa kuzaliwa kupya, ni tofauti sana na hii mipango na madhehebu hata wanasema, "Ah, huyo aonekana kwangu kama mtakatifu anayejigaragaza?" Ona?

79 Si vile aonekanavyo kwako, ni vile Neno la Mungu lisemavyo juu yake. Tazama siku ya Pentekoste, hayo yangeonekanaje? Tazama wakati mwingine walipopokea Roho Mtakatifu; ingeonekanaje? Wanawake na wanaume, bikira Mariamu, na wengine wote, wakiweweseka kama watu waliolewa, wakipepesuka tu, wakilia kwa sauti kuu, kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine, wakiendelea kama kundi la majuha. Lakini walikuwa wakijifia wenyewe, na Roho Mtakatifu alikuwa akiingia ndani yao. Nao waliuwasha moto ulimwengu uliojulikana. Kile tunachohitaji leo ni watu watakaojifia

wenyewe, na waoze wao binafsi, na kuteketeza kila daraja nyuma yao, na kujitolea kwa kila kitu kwa Kristo.

80 Wamwona Roho Mtakatifu akimzungumzia shetani aliye katika mfalme huyu? Tazama mtu huyu ni nani anayemtawala mfalme huyu.

Je, mwakumbuka yale nilisema asubuhi hii, mke wangu aliyosema kuhusu wanawake hawa juu pale, kundi lote la wanawake waliovalia nguo chafu, zinifu? Ona? Kasema, "Bila shaka hawana akili timamu. Mwanamke aliye na akili timamu hangejionyesha mwenyewe hivyo."

81 Nilisema, "Mpenzi, yeye ni Mwamerika tu; hivyo tu. Hiyo ndiyo desturi hapa. Watalifanya, kwa sababu ni desturi." Ona, wanaenenda kwa elimu zao. Lakini elimu zao, ukifuata kichwa chako, unaongozwa na shetani. Shetani alichukua kichwa cha mwanadamu, Mungu huchukua moyo wa mwanadamu. Shetani anakufanya utazame kitu unachoweza kuona. Unasema, "Vema, naam, naam, kuwazia, kutoa hoja." Lakini Biblia hutufanya tutupilie mbali ubishi, na kwa imani twaamini vitu ambavyo hatuvioni. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo ajapo juu ya moyo wa mwanadamu.

82 Katika bustani ya Edeni shetani alichukua kichwa cha mwanadamu; Mungu akachukua moyo wake. Na huo ndio kiti cha enzi cha Mungu, ambapo Mungu anakaa katika moyo wa mwanadamu. Na sasa, kama ni elimu...Hakika, basi mwanaume au mwanamke aliyezaliwa na Mungu atatenda kama Ufalme anaotoka. Haleluya! Hilo lingenifanya nipaze sauti. Mbona? Kwa sababu unapojua ya kwamba umepita toka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu unachukia dhambi, na unampenda Mungu; na utasimama haidhuru kama unakufa ama haufi. Utashikilia kuwa si sahihi, na kuita kibaya kibaya na uenende mwaminifu mbele za Mungu. Inaonyesha kuwa Roho yako, Uzima ulio ndani yako anatoka mahali pengine, ambapo ni patakatifu, na pasafi, na peupe, na pasipotiwa najisi.

83 Na unasema, "Uponyaji wa Kiungu?" Hakika! Roho Yangu inatoka mahali Mponyaji wa Kiungu alipo. Sisi tunatoka kwenye nchi ya uponyaji wa Kiungu. Amina!

84 Kasema, "Je, waamini Mungu yuko." Hakika, inatoka kwenye nchi Mungu aliko. Nasi tu wasafiri na wageni kama Ibrahimu na Isaka. Wakati tu kule—kule kufunikwa kama uvuli na Roho Mtakatifu kulipowagusa, walienda kote nchini wakikiri kuwa wao ni wasafiri na wageni. Walikuwa wakiutazamia Mji ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga ni Mungu. Na sasa, baada ya sisi kupata Ushuhuda kwamba anakaa ndani yetu sisi, zaidi vipi, je, itupasavyo sisi kuwa wasafiri na wageni, tukitembea duniani kote, tukigeuza vichwa vyetu toka kwa vitu viovu, kwa sababu sisi tu taifa lingine, watu wengine. Bila shaka!

85 Sasa tazama maovu ambayo yanautawala ulimwengu huu sasa, tunaposoma Ezekieli 28:12.

> *Mwanadamu, umfanyie maombolezo mfalme wa Tiro, umwambie, Bwana MUNGU asema hivi,* . . . (Sasa tazama; Yeye ananena na pepo aliye ndani ya huyo mfalme. Ona?) . . . *Bwana MUNGU asema hivi; Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima,* . . . *na ukamilifu wa uzuri.* (Shetani, mwaona pale jinsi Shetani alikuwa mzuri sana kati ya wale malaika wakuu?)
>
> *Ulikuwa ndani ya Edeni* . . .

86 Naam, mwajua Mfalme wa Tiro wakati huo haingaliwezekana kuwa alikuwa katika Edeni, maana ilikuwa miaka elfu nne mbele ya hayo. Ona? "Ulikuwa ndani ya Edeni," Yeye ananena na nani? Yeye ananena na Shetani katika mfalme huyo. Haleluya! Ndugu, najisikia wa kidini. Wakati . . .

87 Ndiposa watu hawa watafanyaje wanaomkufuru na kuwadhihaki watu chini ya utendaji wa Roho Mtakatifu? Wanapowafanyia mzaha watu hao wanamkufuru Roho Mtakatifu ambayo haisamehewi kabisa. Wewe haumzungumzii mtu huyo, unaongea na yule Roho anayetenda kazi katika mtu huyo. Yatubidi kuheshimiana sisi kwa sisi, na kupendana, na kufarijiana, kuongea mema sisi kwa sisi. Hilo ndilo litupasalo kufanya.

Sasa sikia haya. Vema.

> . . . *Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima,* . . . *ukamilifu wa uzuri.*
>
> *Ulikuwa ndani ya* . . . *Edeni, bustani ya Mungu, kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki, na yakuti manjano,* . . . *na zabarajadi,* . . . *na shohamu, na yaspi,* . . . *na yakuti,* . . . *ana zumaradi, na baharamani,* . . . *na dhahabu; kazi ya matari yako;* . . . *na filimbi zako ilikuwa ndani yako; katika siku ya kuumbwa kwako zilitengenezwa tayari.*

88 Huyo ndiye yule Nyota ya Alfajiri. Yeye wakati mmoja aliishi katika Edeni. Sasa, tutarudia hilo swali katika dakika chache, yule Nyota ya Alfajiri katika Edeni. Sasa, tutarudia hilo swali katika dakika chache, yule Nyota ya Alfajiri katika Edeni, kwa sababu tuna mbegu ya nyota chini hapa mahali fulani ambalo ni jambo la kutaka uangalifu mwingi. Nilidhani ningetumai tu hilo litakuwa karibu mwisho.

89 Lakini yeye alikuweko, na shetani alifukuzwa toka Mbinguni. Na kusudi lile lile alilojaribu kutimiza Mbinguni, yeye alishuka chini hapa duniani na alikuwa anajaribu awezavyo kutekeleza kile yeye alichokusudia. Yeye huenda kwa wafalme na kwa watawala, na anapowapata, kisha yeye arudi tena kanisani na kuwapata watu—au kuwakuta wahubiri. Kisha

toka kwa wahubiri, yeye aingia moja kwa moja katika kusanyiko na kuingiza kusanyiko chini ya ushawishi uo huo, shetani yule yule akitenda mambo yale yale. "Wajua, wewe ni Mpresbiteria, hutaweza kamwe kuwa mtakatifu anayejigaragaza. Wewe u *hiki, kile au kinginecho;* hungeweza kujiaibisha mwenyewe kwa kuwa kati yao. Naam, unajua vema zaidi ya kuketi kati ya moja ya hayo maskani madogo makuu-kuu ya kale au hiyo misheni kwenye njia ya mji. Naam, watu hao wamerukwa na akili zao." La, sivyo. La, hawajarukwa na akili; wako tu mioyoni mwao; hivyo tu. Hawajarukwa na akili zao; wanatawaliwa tu na mioyo yao. Mungu aishi mioyoni mwao, nao ni watu wa kipekee, ukuhani mtakatifu, wakitoa dhabihu za kiroho; hayo ni matunda ya midomo yao yakitoa sifa kwa Mungu, au wanajisikia hivyo au la. "Wakati mwingine simwoni Yeye," alisema yule mwandishi wa wimbo, "Namtumaini na kumpa Yeye sifa."

90 Kasema, "Vema, ningeenda kanisani, nami ningemsifu Bwana kama ningejisikia kufanya hivyo." Vema sasa, kuhani kazi yake ni kutoa dhabihu. Nanyi, kusanyiko, ni kuhani wakuu kwa Mungu, mpate kutoa dhabihu za kiroho; hayo ni matunda ya vinywa vyenu kumtolea Mungu sifa.

91 Unaenda chini na kusema, "Vema, ningalitaka, ningeenda na kumshuhudia mtu fulani." Vema, fanya hivyo haidhuru! Kama wewe u kuhani mkuu ndugu, inawasha moyoni mwako, endapo unajisikia kama unataka kufanya hivyo au la. Nenda kafanye hivyo tu haidhuru, kwa sababu yakubidi utoe dhabihu, kitu ambacho ni kigumu kukifanya. Enda ukifanya hivyo haidhuru, ninyi ni ukuhani wa kiroho, watu wa kifalme, mkitoa sifa kwa Mungu, kwa sababu Mungu yuaishi humu moyoni.

92 Sasa, kama wewe u wa Shetani, unajisikia u bora kuliko tabaka hiyo ya watu. Sasa, utajuaje ipi ni sahihi? Ilinganishe na Maandiko. Kama mtu amezaliwa na Mungu, yeye huamini kila Neno Mungu aliloandika, na husema Yeye yu mkuu leo kama Yeye alivyowahi kuwa, na Yeye habadiliki, na Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama yeye amejazwa na Roho Mtakatifu, ana Roho Mtakatifu yule yule ambaye Yeye alimtoa kwenye siku ya Pentekoste, na anamfanya atende vivyo na kufanya mambo yale yale. Kama yeye amezaliwa na Roho wa Mungu, Marko 16, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kweli! Kwa hivyo yeye akisema, "Mimi ni mwamini," na ishara hizo hazifuati, basi yeye ni anayejifanya mwamini, si mwamini.

93 Kuna tabaka tatu za watu, mwamini, anayejifanya mwamini, na asiyeamini. Na hizo ndizo tu tabaka tatu pekee zilizoko. Wengi wanaojifanya waamini; kunao wengi walio waamini halisi, na kunao wengi wasioamini. Lakini kama wewe u mwamini halisi, Yesu alisema, "Ishara hizi zizitafuatana na hao waaminio. Kwa Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya. Wakimkanyaga nyoka (Ndugu Evans) haitawadhuru.

Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya!" Ee, hilo ni kweli tu kama Neno la Mungu lilivyo kweli. Hatuna shughuli kuondoa lo lote toka kwalo. Biblia ilisema atakayeondoa wala kuongeza kwa Neno hili, huyo ataondolewa toka kwa kile Kitabu cha Uzima, kwake. Mungu ni mkamilifu sana, hata kila neno lazima liwe kamilifu na lazima litoke Mwanzo mpaka Ufunuo vivyo hivyo, kila neno, kila sheria ya Mungu. Sasa, unaweza kulifanya liseme kitu fulani hapa na kulivuruga hapa.

94 Siku moja nilikuwa nikiketi chini ya mti na Ndugu Charlie juu pale na Ndugu Wood hapa: tulikuwa tukiwinda chini kule Kentucky. Tulikuwa tukiwinda kwa bunduki. Nami. . . Ndugu Charlie na Ndugu Wood walipiga shabaha zao asubuhi hiyo. Kwa karibu yadi 50 walikuwa wakipiga shabaha mahali padogo karibu ukubwa huu mzunguko, pakubwa kama kuchakulo. Wao walisema, "Vema."

95 Nami nilienda pale. . . Nilikuwa nikipigilia vijiti umbali wa yadi 50. Nami nilikosea jicho la kuchakulo na kumpiga risasi kwenye shavu. Nilisema, "Hiyo si halali; bunduki yangu imeharibika." Na ndipo nikaona wasiwasi siku nzima. Jioni iliyofuata nikaenda mapema. Nilipiga risasi magamba ya risasi. Ninge. . . Ilipiga kidogo, nusu inchi upande wa kulia. Naam, ilipiga yule kuchakulo kichwani haidhuru.

96 Kwa hivyo Charlie na wengine, asuhuhi iliyofuata alikuwa juu pale, huku bunduki zile zi—zinavuma tu, zikipiga kuchakulo, nami nikiketi nyuma ya mti nikisugua mikono yangu, nikisema, "Lo, hii bunduki yangu imekuwaje?" Nilijionea aibu, hata nikapiga magoti, nikasema, "Bwana Mungu, sijui imekuwaje kwangu. Mbona ukanifanya nipate wasiwasi mwingi hivi? Mbona niwe hivi? Hao watu wakipiga kuchakulo risasi sana; tayari wamewapata kuchakulo wengi; na mimi hapa, nimeketi nyuma ya mti, nikisugua mikono yangu, nikishangaa, 'Bunduki ya—yangu hailengi shabaha, umbali wa yadi hamsini!" Nikalia, nimeketi pale kando ya gogo.

Ndiposa Roho Mtakatifu akaja, si kwa sauti, lakini Ufunuo, kasema, "Nilikufanya hivyo kwa kusudi fulani."

97 Kwa nini? Siwezi kuchukua Biblia ikisema kitu fulani hapa, kama kanisa lasema, "Roho Mtakatifu alikuwa tu kwa ajili ya kundi lile nyuma kule," kanisa lasema hivyo; na Maandiko yasema, "Ye yote atakaye." Siwezi kufanya hilo lilenge shabaha.

98 Siwezi kufanya Ukalvini—mwamini tu Bwana na una usalama wa milele—na Uarmenia. "Kuwa nisipogusa, nisiposhika, nisipoonja, ni—ningependa kufanya hivyo, lakini siwezi!" . . . Uarmenia uko mbali sana na Ukalvini, na yote mawili yamekosea. Sina budi kuona ambapo. . . Wote wana Maandiko, lakini hawana budi kulenga shabaha. Sasa, kama Mungu alisema jambo fulani katika Biblia hii, halina budi

kulenga shabaha; halina budi kufanya kila mlio katika Biblia hiyo moja kwa moja mpaka katikati hasa ya shabaha. Ni lazima lifanye hivyo, kwa sababu ni Neno la Mungu; na Yeye hana kikomo, hawezi kubadilika. Amina! Napenda hio, kwa sababu hapo waweza kutulia kikamilifu umetosheka kuwa ni Neno la Mungu la milele. Na kwa hivyo, nitajaribu kulichunguza kwa Maandiko mbalimbali kulifahamu—kuona kile lingesema.

99 Shetani alifukuzwa waziwazi Mbinguni na yule Malaika mkuu Mikaeli pamoja na Mungu. Kisha akatupwa duniani, akaja duniani, akaingia katika nyoka, akamdanganya Hawa, ndiposa ameingia katika wanaume, wanawake, katika zamani zote na kuendeleza jambo lile lile aliloanzisha mwanzoni—ufalme mkubwa mno, mzuri kuliko wa watu wengine, awe mtawala juu ya yote, anayejua yote. "Dhehebu letu ndilo kuu sana; lina—lina nguvu juu ya mengine."

100 Mmewasikia wakisema, "Naam, tuna wahubiri mamia kadha katika dhehebu letu. Tuna makanisa makubwa zaidi mjini." Neno pekee linaloendeleza kwangu katika herufi ni S-h-e-t-a-n-i. Naam, hilo kwangu lamaanisha shetani. Unapokuta watu watakaojitenga na kuunda dhehebu, na kuvunja undugu, na kusema hawatahusiana kamwe na lile kanisa ndogo . . .

101 Sijawahi kumwona bado mtu aliye chini sana, au bado sijawahi kumwona mtu aliye mbali sana dhambini; sijamwona mwanamke mmoja ali—aliyeanguka zaidi au mwanamume mmoja aliyeanguka sana, ila yule ningemwendea, na kumkumbatia, na kumwondoa mle nikiweza. Sijawahi kuona kundi la watakatifu wanaojigaragaza au lo lote utakalo kuwaita, wakishangilia, na kuruka-ruka, na kupiga kelele, au lo lote ambalo huenda wakatenda, ila ambapo nitaingia ndani mle na kupiga kelele, na kuruka-ruka, na kupiga shangwe pamoja nao kumtukuza Mungu (naam hasa!) awe mweusi, majano, hudhurungi, mweupe, au vyo vyote vile alivyo. Naam, bwana!

102 Roho Mtakatifu huja kwa hali moja sawa; hiyo ni unapotekeleza matakwa ya Mungu. Kama utawahi kumpokea, utafikia kiwango hicho cha Mungu na si mawazo yako mwenyewe kuhusu hilo. Shetani hujaribu kulifanya la kielimu, kitu kikubwa, watu wakubwa, walioelimika. Yakubidi utupilie mbali mawazo hayo na uamini yale Neno lisemayo kuhusu hilo. Amina!

**80.** Sasa, hapa kuna lingine; hebu tuone ni nini. Vema. **Tafadhali fafanua ule mfano wa wale wanawali watano. Je, Mkristo hufanya dhambi?**

103 Sasa, ule mfano wa wale wanawali watano—ama wale wanawali kumi ni, niwieni radhi. Wale wanawali kumi wanapatikana katika Mathayo 25:1. Wale wanawali kumi walienda kumlaki bwana arusi (sasa tazama!) na watano wao walikuwa wenye busara na walikuwa na mafuta katika taa

zao, watano walikuwa wapumbavu na hawakuwa na mafuta katika taa zao. Hata walipokuwa wakisinzia, mwi—mwito ukaja, "Tokeni mwende kumlaki bwana arusi." Na wale waliokuwa na mafuta katika taa zao, wakazitengeneza taa zao, na moto ulikuwa ukiwaka, nao wakaondoka kwenda kumlaki bwana arusi. Wengine wakaja kununua mafuta, nao waliwaambia waende wanunue toka—mafuta kwa hao walioyauza. Nao walipokuwa wakienda, bwana arusi akaja na—na wale—wale wanawali wenye busara wakaingia, na wanawali wanaolala wakatupwa nje.

104 Hili litaumiza, litaumiza kabisa, lakini yanibidi niseme tu. Mimi sikuuliza hili swali: Ninahusika tu kwa kulijibu. Sasa, hili laja karibu sana, ndugu, karibu sana, hata natumai kuwa litasaidia badala ya kuumiza. Mara kwa mara huna budi kuumiza . . . Kama mama alivyokuwa akisema alipokuwa akinipiga, yeye alisema, "Yabidi kikuumize kabla ya kukufaidi." Vema, hiyo ni—ni kweli. Ona? Singeliona wakati huo, lakini ni—ninaliona sasa.

105 Tazama, ile . . . Hao kumi wote walioenda kule walikuwa wanawali. Sasa, kulikuwa na wanawali kumi walioenda kumlaki Bwana. Sasa, neno lile *wanawali* maana yake ni "waliotakaswa (kuna mtu anayejua hilo?), watakatifu, wasafi, waliotakaswa." Kumi walienda kumlaki Bwana.

106 Sasa kumbuka, walikuwa wakilala katika kukesha kwa kwanza, kukesha kwa pili, kukesha kwa tatu, na kuendelea hadi kukesha kwa saba. Lakini hawa walienda hakika kumlaki Bwana. Na kumbuka, walipokuwa wakienda, Bwana akaja. Huo ulikuwa ule wakati wa kuja kwa Bwana. Si nani aliyekuwa katika kukesha kule . . .

107 Yesu alinena ambapo wengine walilala katika kule kukesha kwa kwanza, na wengine katika kukesha kwa pili, na wengine katika . . . Lakini Bwana alipokuja wote wakaamka. Lakini wakati huu, ilikuwa kule kukesha kwa mwisho, kwa sababu waliondoka, kumi, kwenda kumlaki Bwana. Na watano taa zao zilijaa moshi, na hawakubeba mafuta; watano walikuwa na mafuta.

108 Sasa kumbuka, mafuta katika Biblia ni mfano wa nini? Je, mtu ye yote anaweza kusema? [Kusanyiko linajibu "Roho Mtakatifu"—Mh.] Roho Mtakatifu! Basi ungekuwa msafi, na mwadilifu, na uliyetakaswa bila kuwa na Roho Mtakatifu. Kusafishwa umesafishwa . . .

109 Sasa tazama, nitachukua chupa hii. Na iko hapa kwenye zizi la kuku, kisha imejaa uchafu. Naichukua; huko ni kuihesabiwa haki: "Nitamtumia huyu mwenye dhambi." Basi jambo nitakalofanya kama nataka kuitumia, yanibidi niisafishe. Ndiposa, nikiisafisha, naifanyiaje? Nitaitakasa. Neno *kutakasa* kufanya—maana yake ni "kusafisha", linafanana na takatifu.

*Takatifu—takatifu* ni neno la Kiebrania, *takasa* ni neno la Kiyunani. Neno *takasa* maana yake ni "safisha na tenga kwa ajili ya matumizi." Lakini basi, heri wenye njaa na kiu ya haki maana hao watajazwa, ndiposa wanatumikishwa.

110 Vyombo vile . . . Yale maskani ya Agano la Kale, madhabahu yalitakasa vyombo vile, navyo vikatengwa kwa matumizi. Vilipojazwa, vilikuwa katika matumizi.

111 Sasa hapo ndipo ninyi Wanazirini wapendwa, wa thamani, na wengineo, mlikosea. Ona? Sisi sote . . . Mbona mnashindwa? Mbona Pentekoste walikimbia wakawaacha ninyi. Kwa sababu mlikataa kutembea katika Nuru. Hiyo ni kweli hasa. Ona? Bila shaka. Madhabahu ya kwanza niliyopiga magoti kwake yalikuwa yalikuwa madhabahu mazuri ya kale ya Nazarini humu. Mungu awabariki, kanisa zuri, takatifu, safi, lakini mnashikilia sana sheria hadi mnasema, "Lazima ufanye *hili,* na lazima ufanye *hilo*. Lazima ufanye *hili,"* na hamtambui ni neema ya Mungu na unaitwa kwa kuteuliwa. Si yeye atakaye wala yeye apigaye mbio, bali ni yeye arehemuye, yaani Mungu. Ona? Mungu alichagua asili Kanisa kabla dunia haijawekwa misingi (tuna swali kuhusu hilo katika dakika chache. Ona), kuchagua Kanisa tangu awali kabla ulimwengu haujawekwa misingi.

112 Huwezi, kwa kujisumbua, kuongeza mkono mmoja kwa kimo chako. "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa kwanza na Baba Yangu," Ona? Ona, ilikuwa Mungu aliyetoa wito, Mungu aliyevuta, Mungu aliyeweka msingi wa Kanisa. Sasa, unasema, "Ndugu Branham, hilo ni la Kikalvini kabisa." La, sivyo. Sasa, ngoja! Siamini kuwa Mungu humchagua tu mtu na kusema tu, "Haya, nitakutwaa na . . . "

113 Wabaptisti wote na Wapresbiteria husema, "Vema, namwamini Bwana, hainipasi ku—halihukumu dhamiri yangu!" Si ajabu, hamna lo lote la kuwahukumu. Wanasema, "Vema, kucheza dansi hakunihukumu. Kunywa pombe kidogo hakuniudhi." Kwa sababu hamna cho chote ndani humo cha kuudhika "Kufanya mizaha michafu hakunitatizi." Kwa sababu gani? Hamna cho chote ndani mle cha kutatizika.

114 Lakini simtumikii Bwana kwa sababu nadhani Yeye angenitupa kuzimuni kama singemtumikia; namtumikia Yeye kwa sababu nampenda. Namtumikia Yeye kwa sababu kuna kitu fulani ndani yangu. Ukitoka nje na kusema, "Vema, nitaacha kufanya hili kwa sababu kanisa langu haliliamini," unatenda tu kama mnafiki. Naam. Lakini ukilifanya kwa sababu hilo ni—unapenda kufanya hivyo, na—na ni kumtumikia Mungu, na kitu fulani moyoni mwako kinafanya upendo wa Mungu kuwa mkubwa sana kwako kuliko vitu hivi, sasa wewe unaendelea vyema. Lakini hata kama sikunywa pombe, kuvuta sigara, kutafuna, kutukana, kutofanya cho chote, bado ningeenda kuzimuni. Hakika! Ningalijiunga na makanisa

yote, nikabatizwa, na jina langu likawa katika vitabu vyote, kisha nikafanya kazi nzuri, na kuishi maisha mazuri, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, yeye hata hawezi kuona Ufalme wa Mungu." Hiyo ni kweli!

115 Sasa hawa wanawali, kumi wakapoa. Kilichowakwaza watu na Nazarini kilikuwa hiki: Kwa sababu Wapentekoste walishikilia kuwa ishara madhubuti ya Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha. Waliwakusanya madhabahuni na kuwafanya waseme maneno fulani na kuyarudia-rudia hata wakanena kwa lugha. Mpentekoste halisi wa kweli hangekubali hilo. Shetani alikuwa na vitu vingi sana ndani ya kanisa lenu la Nazarini pia. Ona? Na ana vitu vingi sana katika kanisa la Kipentekoste, walakini kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, hiyo ni Kweli. Hiyo ni Kweli hasa.

116 Kunazo nyingi najua. Nimesikia watu wakinena kwa lugha. Siwezi kuhukumu; sikutumwa kuhukumu. Nimesikia nyingi yazo; ilisikika kama shaba iliayo na upatu uvumao. Lakini najua kuna Roho Mtakatifu halisi anayenena kwa lugha. Nami najua hilo ni kweli. Naam, bwana!

117 Lakini waliona watu wakiingia na kusema, "Mungu atukuzwe, nimempokea." Vema basi, hilo ni jambo lile lile... Sasa, usiite hilo la Kipentekoste kwa sababu waliruka juu-chini, na kunena kwa lugha, na ukawaona hao nje kule na mke wa mtu mwingine au na mume wa mtu mwingine.

118 Mwasema, "Hilo ni Roho Mtakatifu?" Ninyi Wanazarini mlipiga shangwe kotekote sakafuni na kutenda jambo lile lile. Mlisema mlimpokea mlipopiga shangwe. Ona? Hakuna njia yo yote unayoweza kulithibitisha kwa—ila kwa maisha unayoishi. "Kwa matunda yao mtawajua." Hivyo ndivyo ilivyo. Maisha ya kitauwa na Kristo akifanya kazi nawe akithibitisha Neno, ishara na maajabu vikifuatana na maisha yanayomcha Mungu, hilo ndilo jambo halisi. Sasa, unaweza kuwa na ishara na nyingi bila maisha yale. Unaweza kuiga maisha yale bila ishara, lakini unapoviona vyote pamoja, basi hiyo ndiye. Ndiye huyo.

Sasa! Ndiposa, kumbuka, Bibi-arusi...Sasa huenda nikamaliza hili kama mna dakika chache tu, kuendelea nalo.

119 Tazama, mwanamke atakata nguo yake. Ana jora kubwa. (Hebu tuiite nini? Kitambaa cha bafta, kitenge au cho chote kile, jina fulani mlilo nalo. Hebu tuseme ni hariri.) Naye ana mshono fulani. Naye atazama hii jora kubwa. Sasa, ni juu yake ataweka wapi huo mshono. Sivyo? Yeye anaweza kuchagua sehemu yo yote ya jora hii, na jora yote imetakaswa, ni safi. Ona, ni uchaguzi. Uchaguzi wa Mungu. Kwa hivyo Yeye afanyaje? Mungu huchukua kwa kuchagua na kuweka mshono huu wa Kristo po pote atakapo kwenye jora hiyo. Kisha inakatwa. Sehemu iliyobaki ya hiyo jora ni takatifu tu kama sehemu hii ilivyokuwa takatifu, lakini kwa chaguo Mungu alifanya

chaguo Lake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Je, Paulo hakusema katika Wakorintho 8 namaanisha—Warumi, 8, kuwa—"Mfinyanzi aweza—udogo waweza kumwambia Mfinyanzi, kwani kuniumba hivi?" Mungu aweza, Aliye mwenye haki, wakati Yeye angemwambia Esau na Yakobo kabla ye yote wa hao wawili hajazaliwa wala hawajatenda neno jema wala baya, "Namchukia Esau na kumpenda Yakobo?" Ni kwa sababu kwa kujua tangu awali Yeye alijua kile Esau alikuwa na kile Yakobo alikuwa. Yeye ajua nini kilicho ndani ya mtu. Kabla ulimwengu kuwekwa misingi Yeye alijua, Yeye . . .

120 Kama ungeeleza neno *pasipo kikomo* . . . Kwa neno *pasipo kikomo* . . . Nasema kumekuwa na tani bilioni mia za mbu duniani (hizo hazingelianzisha), tani bilioni mia za ulimwenguni, na kila mmoja wao amepepesa macho mara triloni bilioni mia. Na hakuna ye yote wao aliyepepesa macho yake ila yule Mungu alijua kabla ulimwengu kuwekwa misingi. Hilo ni lisilo kikomo. Hilo ni namna ya kitu kisicho na kikomo. Ona?

121 Yeye hana kikomo. Kwa hivyo kabla kuwekwa misingi ya dunia Yeye alijua kile ungefanya. Kisha Yeye akamtuma Kristo, si kuwa tu . . . Kama mtu fulani, "Vema, nikiacha tu uchoyo wangu na kumfuata Yeye," au kitu kama hicho, hilo sicho. Yeye alijua nani angeokoka, kwa hivyo akamtuma Kristo kuokoa kile Yeye alichoona hapo mbeleni kingeokolewa. Hiyo ni kweli kabisa.

122 Sasa, Kanisa Lenyewe lina usalama wa milele. Ukiwa katika Kanisa u salama pamoja na Kanisa. Lakini uondokapo nje ya Kanisa, wewe hauko salama. Ona? Sasa, kaa Kanisani.

123 Unaingiaje Kanisani? Kushikanisha mikono, kuandika jina lako kwenye kitabu? Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja; huo ni Kanisa. Vipi? Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu sisi tumetiwa muhuru katika Mwili wa Kristo. Hata lini? Hata siku ya ukombozi wako. Waefeso 4:30, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi." Kutiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Naam. Bila shaka, bila shaka, huyo ni Roho Mtakatifu.

124 Na sasa, Kanisa hilo lilinyakuliwa, na masalio wa uzao wa mwanamke wazishikao amri za Mungu na wana imani katika Yesu Kristo (Ona?), si Bibi-arusi, wasalia wa uzao wa mwanamke. Kisha yule nyoka akatoa katika kinywa chake maji afanye vita na uzao uliosalia. Hapo ndipo wakati kanisa la protestanti chini ya Muungano wa Makanisa, ambao ni sanamu ya mnyama sasa unaundwa . . . Na kutakuwako kususiwa kwa makanisa yote kama hili.

125 Kama mkusanyo huu wa kodi tunaofanya hapa sasa, ubishi, kujaribu kusema kuwa sisi si kanisa, na tuna haki ya Kikatiba kusema sisi ni kanisa. Mradi Katiba ingaliko,

hamna mabadiliko, basi bila shaka tuna haki, haki kama tu mtu mwingine ye yote. Baba zetu waliotutangulia walisimamia hilo. Lakini tumefanyaje, tumevunja kila Katiba ya sheria tunayoweza kuvunja, na hivi punde Muungano wa Makanisa, ambamo makanisa yote na madhehebu yamealikwa kuingia, na shetani ameingia na kufanya ya kilimwengu na kila kitu katika washiriki wa kanisa la mahali pale na mengineyo kama hayo, na makutano makuu na daraja, na shirika, wakati kanisa ndogo la kale bado lingali kule chini likizaliwa mara ya pili katika mchafuko kama kuzaa kwo kwote kulivyo, lingali linalipa thamani, lingali linafifia na kufa, likitenda vivyo hivyo walivyofanya walipozaliwa mara ya kwanza kule kwenye siku ya Pentekoste, kanisa la aina ile ile chini kule . . . Yatafungwa na kukomeshwa chini ya Muungano wa Makanisa. Kutakuwa na kususiwa kama chama au kitu fulani. Au utaingia au utaondoka.

126 Ile chapa ya mnyama iko hivi sasa, na Mu—Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Kuukataa ni chapa ya mnyama. Ye yote yule aonaye Roho Mtakatifu, ambaye wapaswa kumpokea, na humpokei, moja kwa moja unapata chapa ya mnyama, kwa sababu kuna tabaka mbili tu zitakazokuwepo: wale wote ambao hawakuwa na Muhuri wa Mungu walikuwa na alama ya mnyama. Kwa hivyo kupokea Muhuri wa Mungu ni kumpokea Roho Mtakatifu. Kuukataa ni kupata chapa ya mnyama. Hilo ndilo jambo lote. Hiyo ni kweli kabisa.

127 Sasa, Bibi-arusi akapanda juu, masalio wakabaki hapa. Nao ndio watakaofufuka katika ufufuo wa pili. "Heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu yake katika ufufuo wa kwanza, juu ya hao, mauti ya pili haina nguvu." Naam. Ufufuo wa pili utakuwa ile Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi, kisha kanisa . . . "Je, hamjui," alisema Paulo, "mnaenda mbele ya wasioamini na wanasheria na kadhalika hali watakatifu watauhukumu ulimwengu." Mambo haya yabidi yaamriwe mbele ya Kanisa, si mbele ya hakimu wadhalimu na kadhalika, lakini yabidi hoja zetu ziwe mbele ya Kanisa. Pale mnapelekana ninyi kwa ninyi kwa sheria. Na Mungu amhurumie mtu atakayempeleka Mkristo kwa sheria. Naam. Paulo hata aliwaonya wasifanye hivyo.

128 Sasa huyo ndiye Bibi-arusi, na ndio hao wale wanawali wanaolala, wata—watakaobaki duniani. Wanawali wenye busara wanaenda Mbinguni wakiwa na mafuta katika taa zao.

Najua tungechukua muda mrefu kwa hayo, lakini nina—nitaharakisha nimalize haya.

129 "Je Wakristo hutenda dhambi?" Hasha, la! Hakuna Andiko ambapo Mkristo hutenda dhambi. Yeye hawezi kutenda dhambi. Najua hilo linachukiza. Vema, tutaenda tu kwa 1 Yohana 3 na tuone Maandiko yasemavyo. Mkristo hatendi dhambi.

130 Je, mmepata kumwona ndege mweusi, mweupe au ndege mweupe-mweusi? Je, mliwahi kumwona mtu aliyelewa asiye

mlevi? La! Hamjapata kumwona mwenye dhambi mtakatifu pia. Hakuna kitu kama hicho.

131 Sasa, kama hili likichukiza kidogo, tia marhamu ya kutulizia, mwajua, na ita—itaponya katika muda mfupi sasa.

132 Sasa, Maandiko ndiyo yanayothibitisha bila shaka na bila kukosea yale tunayonena. 1 Yohana sura ya 3 na kifungu cha 9. Vema, sikiza hili!

> *Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za ibilisi.*

Sikiza, mko tayari? Vaeni makoti yenu, silaha zenu zote ni tayari? Sikizeni kwa makini kwa sababu hili ni la kushangaza.

> *Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi,*. . . (Hilo likoje?). . .*kwa sababu uzao wake*. . .(Uzao Wake, wa Mungu). . .*Wakaa ndani yake,*. . .(Mtu yule!). . . *wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu.*
>
> *Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa ibilisi nao. Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye*. . .*asiyempenda ndugu yake.*

Wawezaje kuwa na madhehebu na kuweka mipaka na mambo kama hayo, na kusema umezaliwa na Mungu? Hakuna jambo kama hilo. Ni dhihaka za—za Shetani. Hiyo ni kweli. Lakini mtu aliyezaliwa na Mungu hawezi kutenda dhambi; haiwezekani kutenda dhambi.

133 Tazama! Hebu nichukue tu msalaba huu kwa dakika chache kama utatoka pale. Nani alikuwa tolea la dhambi? Yesu Kristo. Tunaingiaje katika Kristo? Nani aliyetufia? Kristo. Yeye alifia nini? Dhambi zetu. Yeye alichukua hukumu yangu. Sivyo? Ndiposa ninaingiaje ndani Yake? Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili mmoja. Na tukiwa katika Mwili huu, tunafunikwa na Damu na tuko huru kwa hukumu. Hawezi kutenda dhambi, kwa sababu kuna dhabihu ya Damu iliyowekwa kwa ajili yake mchana na usiku. Haleluya! Hawezi kutenda dhambi. Hana hamu ya kutenda dhambi. Akiitenda—akifanya jambo fulani baya, hakusudii kulifanya. Biblia ilisema katika Waebrania sura ya 10, "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli (na Yeye ndiye Kweli), haibaki dhabihu kwa ajili ya dhambi. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa alikufa kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyeikanyaga ile Damu ya Yesu Kristo na kuihesabu Damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa kitu ovyo, na kuifanyia jeuri kazi ya neema."

134 Maana kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja nasi tu huru toka kwa dhambi; hatuwezi kutenda dhambi. Kuna utakaso unaotungoja sisi. Na kama kungali kuna hamu moyoni mwako ya kutenda dhambi, hujawahi kubatizwa katika Mwili huo, kwa sababu umekufa na maisha yako yamefichwa katika Kristo kwa Mungu na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Wakristo hawatendi dhambi. Wao hufanya makosa, lakini hawatendi dhambi. Amina! Hiyo ndiyo sababu hawatendi, kwa maana hawezi kutenda dhambi.

135 Nawezaje kuwa na. . .Nikipitia mjini hapa, naye meya wa mji asema, "Bw. Branham, najua wewe huwatembelea wagonjwa. Kuna spidi inayoruhusiwa. Spidi inayoruhusiwa mjini ni maili thelathini kwa saa. Lakini ninakupa wewe ruhusa kuendesha kwa maili tisini ukitaka, sababu nina imani kwako kuwa hutaendesha hivyo isipokuwa umepokea wito wa hatari au mtu fulani anakufa kule ng'ambo kwa ajali ya barabarani. Na nitakupa ruhusa kama meya wa mji huu, kuwa unaweza kuendesha kupita taa nyekundu zo zote, ufanye lo lote unalotaka, endelea tu." Afisa mdogo mwenye tepe mbili angewezaje kunishika nje pale nikiendesha kwa mwendo wa maili arobaini kwa saa katika sehemu ya kuendeshea maili thelathini kwa saa? Hawezi. Siwezi kuvunja sheria zo zote za spidi katika mji huu, kwa sababu gani? Mimi sizuiwi na sheria za spidi. Amina! Natumai mnaliona.

136 Na tunapokufa, na Mungu ametambua kutubu kwetu, Yeye ametambua ubatizo wetu, Yeye ametambua ile Damu ya Mwanawe, ambayo kwa imani imewekwa, Yeye hutambua kuchagulia Kwake tangu awali na alijua kuwa ningefanya hilo, na amenitambua mimi katika Kristo, kufa. . .Na Kristo alikufa badala yangu Yeye alipochinjwa kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Jina langu liliwekwa kwenye Kitabu Chake kama Mkristo. Haleluya! Kristo alikufa kifo changu. Kristo ni Dhabihu yangu. Na Mungu hangenihesabia tena dhambi. Yeye amenipa Muhuri wa Roho Mtakatifu kama ushuhuda kuwa nimepita toka mautini kuingia Uzimani. Whiu! Hilo ndilo jambo muhimu.

137 Ndipo hao waliozaliwa na Mungu hawatendi dhambi, kwa maana yeye hawezi kutenda dhambi. Katika Agano la Kale kila mwaka kulikuwako na ukumbusho wa dhambi. Lakini Kristo, kwa dhabihu moja Yeye amemkamilisha aabuduye milele. "Mwa—mwabudu akiisha kusafishwa mara moja (Waebrania 10)— mwabudu akisha kusafishwa mara moja asingejiona tena kuwa na dhambi." Kwa hivyo wachukue watu hawa wanaokimbia kanisani na kuruka juu chini, na kupasa sauti, na kunena kwa lugha, na kutenda kama Mkristo hasa, na mwaka unaofuata inawabidi kurudi tena, juma linalofuata. Hawajafika mahali po pote tangu mwanzo. Wanaiga tu, maana Biblia ilisema Roho Mtakatifu hututia muhuri katika Kristo

hata siku ya ukombozi wetu. Haleluya! Hilo ndilo linifanyalo niwe na matumaini, kwa sababu Mungu aliahidi hivyo.

138 Hamna dhambi tena. Swali la dhambi limemalizwa. Hiyo ndiyo sababu dhambi huonekana chafu sana kwa Mkristo. Hiyo ndiyo sababu wanawake nje hapa wakiwa wamevalia hizi suruali fupi huonekana wachafu sana, kwa Mkristo. Hiyo ndiyo sababu ushenzi, hayo ni mambo machafu sana, hiyo ndiyo sababu kuvuta sigara, kunywa pombe, kucheza kamari, hivi vipindi vyote visivyokaguliwa kwenye televisheni, upuzi huo wote waonekana mchafu. Mbona? wewe u wa Ufalme tofauti. Umezaliwa katika Ufalme wa Mungu na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu hata siku ya ukombozi.

139 Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, maana yeye hawezi kutenda dhambi, Mbegu ya Mungu iko ndani yake, naye hawezi kutenda dhambi. Mradi tu Roho Mtakatifu yumo ndani mle Yeye huondolea kila tamaa ya dhambi mbali na wewe. Amina! Huwezi kutenda dhambi; hakuna tena tamaa yake.

Tungechukua muda mwingi kwa hilo, lakini hebu tuharakishe. Hatutayamaliza, nasikitika.

**81. Mbona makanisa yanayobatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu na kuwaruhusu wanawake wahubiri, mbona yana nguvu nyingi na mamlaka?**

140 Sasa, hilo ni jambo la kutaka uangalifu mwingi. Sasa, najua kuwa ninaongea na watu ambao hawatakubaliana na hili, lakini kama Mkristo lazima niliseme. Hakuna mamlaka ya Kimaandiko katika Biblia kwa ubatizo wa maji kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hamna hata mtu mmoja aliyewahi kubatizwa katika Biblia kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Hayo ni mapokeo ya Katoliki yaliyoenezwa katika karne sita.

141 Kunyunyizia maji hakukuwahi kuwa katika Biblia, kwa watu kunyunyizia wala kumwagiwa, ila kuzikwa. Ukitaka kujua hilo, hapa nina Kiyunani na Kiebrania pia kulihusu.

142 Na kwenye Siku ya Pentekoste, Petro aliamuru kuwa kila mtu lazima atubu na kubatizwa kwa Jina la Yesu Kristo wapate ondoleo la dhambi zao. Na Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu si jina. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu . . . Mathayo 28:19 ilisema "Basi, enedeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina," si kwa majina, kwa Jina, umoja wa . . . Si kwa jina la Baba, Mwana, na la Roho Mtakatifu; lakini kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. *Baba* si jina; *Mwana* si jina; *Roho Mtakatifu* si jina. Ni vyeo vinavyohusu Jina.

143 Sasa, siku kumi baadaye Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu mkabatizwe kwa Jina lake Bwana Yesu Kristo." Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, tazameni jinsi wazo la waaminio utatu sana . . . Ona, wanajaribu kufanya miungu mitatu toka kwa hilo. Hamna miungu mitatu. Ningependa kuwasomeeni hilo toka

kwa kile Kiyunani asili hapa. Njia pekee waliyobatizia kwa Jina la Yesu ilikuwa, na Biblia ilisema katika Kiyunani asili, ilikuwa kufanya hao watambue kuwa Yeye alikuwa Mungu.

144 Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni afisi za Mungu mmoja, Yeye alikuwa Baba; Yeye alikuwa Mwana; Yeye ni Roho Mtakatifu. Ni afisi tatu au muda mtatu wa wakati, wa Ubaba, Uwana, na majira ya Roho Mtakatifu. Lakini Baba, Mwana na Roho Mtakatifu zina Jina moja, Bwana Yesu Kristo.

145 Kila mtu tangu siku hiyo alibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo, nao waliwakuta wengine ambao hawakubatizwa kwa Jina lo lote, na Kiyunani cha asili kilisema papa hapa na hata Kiebrania, kuwa ubatizo kwa Jina la Yesu ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi, Kiyunani na Kiebrania pia. *Kuondoa* maana yake ni "kusamehe," bila shaka. *Nikiondoa* kitu cho chote, ni kukifutilia mbali. *Kuiondoa*—"kuifutilia mbali."

146 Lakini hakuna Andiko katika Biblia. . .Na mtume Paulo alipitia kule akapata ndugu kadha Wabatisti, Matendo 19. Walikuwa na wakati mkuu na kadhalika; Walikuwa wakihubiri, shangwe; walikuwa na furaha katika kambi.

147 Akila na Prisila katika ile sura ya 18 walikuwa wamewatembelea watu hawa, Apolo; walikuwa Wabaptisti. Na Paulo akawaendea, naye akawauliza, "Mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Nao walimjibu, "Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu ye yote."

148 Yeye alisema, "Mlibatizwa kwa ubatizo gani?" Najua katika nakala ya King James inasema "mlibatizwaje": katika ile ya asili ilisema, "vipi." "Mlibatizwa vipi au namna gani?"

149 Wao walisema, "Tumebatizwa na mtu yule yule aliyembatiza Yesu, Yohana." Paulo akasema, "Huo haufai tena. Hamna budi kubatizwa tena." Nao waliposikia haya, wakarudi majini wakabatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Paulo akawawekela mikono yake, kisha Roho Mtakatifu akaja juu yao. Sasa, kama hiyo—kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, inasema hapa, na Bwana Yesu Kristo, inasema hapa, yote mawili hayawezi kulenga shabaha. Haina budi kuwa kweli.

150 Sasa, katika Mathayo 28:19, hiyo ndiyo sura na kifungu cha mwisho katika Mathayo. Kama ukisoma hadithi ya mapenzi, nayo ilisema, "Yohana na Mariamu wakaishi raha mstarehe," Yohana na Mariamu ni akina nani? Rudi mwanzoni mwa hicho kitabu; chunguza wao ni nani. Chunguza hao Yohana na Mariamu walikuwa nani walioishi raha mstarehe. Kama Yesu alisema, "Enendeni mkabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," na *Baba* si jina, *Mwana* si jina, na *Roho Mtakatifu* si jina, basi alikuwa akisema nini? Ni nani Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu? Rudi mwanzoni mwake ukasome.

Nitanukuu kutoka ukoo wa Yesu Kristo, sura ya 1, kifungu cha 18:

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi:*. . .(Sasa tazameni kwa makini Sana. Ule mwimo, tutauita *Baba,* mimbara hii, *Mwana,* hiki, *Roho Mtakatifu.* Basi, Baba ya Yesu Kristo ni nani? Ni Mungu. Nyote mnakubali hilo? Mungu ndiye Baba wa Yesu Kristo. Huo ni Mungu Baba. Hii ni Mungu Mwana. Kile ni Mungu Roho Mtakatifu.)

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo*. . .*hivi*. . .(Mathayo 1:18) *Mariamu*. . .aliolewa—*Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa*. . .([Kusanyiko linasema "Roho Mtakatifu"—Mh.] Nilidhani Baba Yake alikuwa Mungu. Nilidhani alisema eti Baba Yake alikuwa Mungu. Basi inawezekanaje kwa wote wawili Mungu na Roho Mtakatifu kuwa Baba Yake, iwapo wao ni watu wawili mbalimbali, nafsi mbili mbalimbali, utu, vyo nyote unavyotaka kuiweka? Hawana budi kuwa Mtu yule yule, ama Yeye alikuwa na baba wawili wa kiroho.)

> . . .*kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Mariamu*. . .*mama yake*. . .*ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa*. . .(si wa Mungu Baba, bali wa). . .*Roho Mtakatifu.*

> *Na hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe was nabii akisema,*

> *Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana;*. . .(Ona?). . .*nao watamwita jina lake Imanueli;* ambalo maana yake ni, *Mungu pamoja nasi.*

151 Naye aliitwa Jina Lake nani? Yesu, Vema. Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Sasa, Baba na Roho Mtakatifu ni Roho yule yule. Roho ni nini? Ni Roho wa Mungu. Na ilivyokuwa, Yeye alikuja katika ubatizo wa Yesu akakaa ndani Yake, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa kukaa ndani Yake." Yeye alishuka akaishi katika Yesu, na hiyo ikamfanya Imanueli duniani. Kwa hivyo Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni nini? [Kusanyiko linajibu, "Yesu Kristo!"—Mh.] Bila shaka lilikuwa hilo.

152 Kwa hivyo Petro alikuwa na ufunuo ule ule. Sasa, tumekazia macho yetu. Tunalenga katikati hasa ya shabaha. Hebu tuone kama wanafunzi walipiga risasi hivyo. Kila wakati walipokuja pamoja, kila wakati ubatizo ulipotajwa, ilibidi wabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo, maana Yeye alisema, "Kwa maana hapana Jina lingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Ni mawazo ya uongo ya shetani na hakuna Andiko lo lote kwa hayo. Naam.

153 Na sasa, natumai hilo halikuumiza, lakini ni Kweli. Ona? Ni Kweli, ndugu. Huwezi kufanya hilo . . . Huwezi kulenga Baba, Mwana, Roho Mtakatifu mahali pamoja na Yesu pengine, wakati hakuna ye yote aliyewahi kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Kila mtu katika Biblia alibatizwa kwa Jina la Yesu, na wale hawakubatizwa hivyo ilibidi waje na wabatizwe tena kabla hata hawajampokea Roho Mtakatifu. Huenda wakatenda kana kwamba wana nguvu sana. Yakubidi ufuate ule mpango usiokoma wa Mungu. Naam. Vema.

154 Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni kosa. Sasa, kwa wanawake wahubiri, kila mtu ajua hilo ni kosa, kama hujui zaidi ya hilo! Laiti ningalikuwa na wakati wa kusoma hayo kwa Kiyunani hapa, yale kilisema, "Ninyi wanawake mkitaka kujua lo lote, na wawaulize waume zao, kwa sababu ni aibu na fedheha kwa mwanamke hata kunena kanisani." Kiyunani chasema hivyo—namaanisha, Kiebrania. "Kama pia isemavyo torati na wawe watulivu na wamtii mchungaji wao kwa kila namna (ona?), kwa maana ni dhambi na aibu kwa mwanamke kunena kanisani." Salale, mtu ye yote apaswa kujua hilo. Na sasa . . . Na kotekote Maandikoni, na Timotheo, na Maandiko mbalimbali, nimeyaandika hapa, ni Ukweli. Vema.

155 Sasa, basi mbona wana nguvu? Mwasema, "Mbona hilo lafanyika?" Tazama ndugu, hebu nikuulize, ama dada, ye yote yule aliyeuliza swali hili. Nimeona baadhi ya mikutano yenye nguvu zaidi kati ya Waislamu, wakilia, wakiruka-ruka, wakichukua kisu na kuchoma moyo wao hivi, na kuumwagilia maji kutoka nyuma, wakatembea kupitia motoni wakali miguu mitupu, kila kitu hivyo, walale kwa kitanda cha miiba, na—na wachukue upanga na kuuchomelea vinywani mwao na kuuchomelea hivyo—unaweza kuuchukua wewe mwenyewe na kuuchomoa, na damu juu yake na kadhalika. Usinene kuhusu mambo hayo. Ona? Hilo si Kweli; hilo halithibitishi lo lote. Ona? Yesu alisema . . . Hebu niwasomeeni Maandiko niliyowaandikieni hapa, Mathayo 7:21-23: "Wengi watanijia siku hiyo . . . Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika huo Ufalme; bali ni hao wafanyao mapenzi ya Baba Yangu aliye Mbinguni watakaoingia. Kwa maana wengi watanijia siku hiyo na kusema, 'Bwana, sikuhubiri kwa Jina Lako. Sikutoa pepo, na kufanya unabii, na kufanya mambo haya mengineyo'". Yeye atasema, "Ondokeni Kwangu, enyi watenda maovu, hata sikuwajua ninyi." Ona?

156 Kwa hivyo usi . . . Ona, Ukweli unaweza kuja tu kwa njia moja, Ndugu. Sasa, sisemi kuwa watu wanaobatiza kwa Jina la Yesu Kristo wote wataenda kuzimuni. Sisemi hivyo. Mungu ndiye Hakimu; mwache Yeye afanye lo lote apendalo, lakini hakuna Andiko halali katika Biblia kwa mtu ye yote kubatizwa kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

157 Paulo aliamuru kila mtu aliyebatizwa kwa njia nyingine yo yote isipokuwa kwa Jina la Yesu aje akabatizwe tena kwa Jina la Yesu, na akasema, "Malaika akija kutoka Mbinguni na ahubiri fundisho lingine lo lote (Wagalatia 1:8), na alaaniwe." Na Paulo alisema, "Kama nilivyosema mbeleni nasema tena, kama malaika akitoka Mbinguni ambaye angehubiri kwenu jambo lingine lo lote na alaaniwe."

158 Sasa, hilo haliwezi. . .Huwezi kupiga shabaha hapa na kupiga shabaha pale. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, useme, "Waache waende zao, wako sahihi!" Na Jina la Yesu, uache hilo liende na kusema, "Wako sahihi." Yabidi kuwepo kitu fulani ambacho kitapiga shabaha vilivyo. Mungu si mwanzilishi wa machafuko.

159 Na ukaufuatilie huo kotekote katika Biblia po pote utakapo, na utaona kuwa ni ubatizo wa uongo. Kisha kaiendee historia, na hadi kwa karne ya sita wakati Agtobus mkuu, naamini ni yeye, aliyebatiza au mmoja wa wale. . .Singesema ilikuwa Agtobus; nasahau jina lake lilikuwa nani aliyebatiza . . . Ukitaka kulipata katika kile—kile *Wazee Kabla ya Nikea* mbele ya, kabla—mkutano wa Nikea, 325 A.D. walikuwa wakali wanabatiza kwa Jina la Bwana Yesu. Na kanisa Katoliki lilipochukua mamlaka walichukua jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Hapakuwepo kamwe wakati mmoja tangu hapo kurudi nyuma, ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ni mapokea ya Katoliki.

160 Luther alibeba mengi sana alipoondoka. Wesley akabeba yaliyobakia, sisi bado tunayaendea. Na ile katekisimu ya Katoliki, ile inayoitwa *Imani Ya Baba Zetu*, naamini inaitwa hivyo, ukurasa wa 144, nadhani ni hapo, yeye alisema—walisema, "Je, Mprotestanti ye yote ataokolewa?" Kasema, "Labda baadhi yao. Wanadai wanaishi kwa kufuata Biblia, lakini bado wanachukua mafundisho ya Katoliki." Kasema, "Biblia, wale Wakatoliki wengine, walibatiza kwa jina la Baba—kwa jina la Bwana Yesu Kristo, lakini sisi tumeondoa utaratibu huo na kuufanya Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, na Waprotestanti wanautambua." Kasema, "Labda wengine wao wataokolewa." Si kwa hilo, hawawezi! Vema.

**82. Kuna zaidi ya ulimwengu mmoja?**

161 Naam, kunazo dunia za dunia, Waebrania sura ya 1 kifungo cha 2, Waebrania sura ya 11 na kifungu cha 3. Kunazo dunia za dunia. Mungu aliumba dunia nyingi, d-u-n-i-a n-y-i-n-g-i, dunia nyingi.

**83. Kunazo zaidi ya mbingu moja?**

162 Naam, katika I—katika II Wakorintho 12:3. Paulo alisema yeye alimjua mtu aliyenyakuliwa juu mpaka mbigu ya tatu. Na katika Ufunuo na kwingineko, kunazo zaidi ya hizo. Sina budi kuharakisha, kwa sababu hivi—hivi sasa umepita wakati wangu

wa kumalizia. Ingekuwa vema kama ningesoma haya mengine yaliyobaki na (vema) kueleza kidogo tu?

**84. Je, mtoto mchanga katika Kristo atanyakuliwa?**

163 Bila shaka iwapo yeye ni mtoto mchanga aliyezaliwa mara ya pili. Haidhuru yeye ni mchanga vipi, atanyakuliwa haidhuru. Mwaona?

**85. Mbona ilimbidi Kristo alinitokea nilipokuwa karibu kupokea Sakramenti?**

164 Vema, hapana shaka moyo wako ulikuwa katika hali safi na ulikuwa ukimjia Mungu kwa unyenyekevu kuipokea; na hiyo ndiyo sababu Yeye alikutokea. Ona, hiyo ndiyo sababu pekee niijuayo. Singesema zaidi ya—ya hayo . . . Hebu tuone.

**86. Kama tuliokolewa kabla kuwe . . .** (Ee, ee. Hatutaki kukomea hapa sivyo?) **Kama tuliokolewa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu—sivyo?**

165 Naam, bwana! Ufunuo 13:8 ilisema kuwa uliokolewa na jina lako liliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla Ulimwengu haujaumbwa. Na Waefeso 1:4 na 5 . . . Hebu nisome hilo; halitachukua ila dakika chache na mtaona kuwa mimi siko tu—tu kulinukuu, mimi—mimi . . . Vema, ndicho hiki; hebu tukisome hiki.

> *Atukuzwe Mungu, Baba* . . . (Waefeso sura ya 1 kifungu cha 3)
>
> *Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo Yesu:*
>
> *Kama vile* . . . (Sikiza!) . . . *Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake* . . . (Kama Kristo alivyotufia sisi, bila shaka.)
>
> *Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake.*

166 Sasa, katika kile Kitabu cha Ufunuo . . . Nina hicho hapa; Hebu nikipate upesi, ili ninyi—ninyi mwone kuwa sikukinukuu tu. Nataka kukinukuu. Ufunuo 13:8, sikiza hili upesi.

> *Na watu wote wakaao juu ya nchi ambao majina yao—juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana—Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.* (Ilikuwa wakati huo. Vema.)

**87. Je, tu—tulikuwa roho wakati huo?**

167 La, hatukuwa hata kitu wakati huo, lakini tulikuwepo katika mawazo ya Mungu. Na yeye akanena na ikawa. Yesu alichinjwa kabla . . . Wangapi wanajua kuwa Biblia yafundisha

kuwa Yesu Kristo alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Kwani? Mungu alinena na Yeye aliponena, ilikuwa tu kama lililomalizika. Na Yeye aliponiona mimi, alikuona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, tulikuwa tu katika mawazo Yake kwa mfano. Ndipo tulipokuja ulimwenguni, tulikuwa wanaume na wanawake pamoja, wa kiume na wa kike. Yeye alitenganisha roho ya kike toka kwa mwanamume na akaifanya kuwa mwanamke na akaifanya kuwa mwanamke na kuiacha ile roho ya kiume ndani ya mwanamume.

168 Unapoona mwanamke akitenda kama mwanamume, kuna kasoro fulani. Mkimwona mwanamume akitenda kike kama mwanamke, kuna walakin.

169 Ndiposa Yeye akatoa ubavuni mwa mwanamume na kumfanyia msaidizi, nao hao wawili ni mmoja.

170 Lakini kabla ya kuwekwa misingi ya dunia majina yetu... Mwana-Kondoo alipochinjwa, majina yetu yaliandikwa kwenye kile Kitabu, wakati Mungu katika mawazo Yake alituona kimbele na kutuchagua tangu asili kwa kujua Kwake tangu awali kabla kuwekwa misingi ya dunia. Ee, ndugu, kama hilo halitalifanya kanisa liamke na kukimbia kwenye marefu ya kanisa? Wazia hilo. Ninyi mliozaliwa mara ya pili, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, Mungu aliandika jina lako kwenye kile Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Kristo alikufa na kumtuma Roho Mtakatifu hapa kukuitia wewe Uzima wa Milele. Umeupokea; Yeye amekutia muhuri. Wewe uko pale hata siku ya ukombozi wako. Haleluya!

171 Nena kuhusu kushikilia. Sio, je, ninashikilia; ni, Yeye alishikilia. Si kile nimefanya; ni kile Yeye ametenda. Sio eti, niliacha kuvuta sigara; niliacha kusema uongo; niliacha kuiba; ni kwamba Yeye aliyenifia. Naye akatoa roho yangu kwangu na kuniokoa nipate kuwa kiumbe kipya.

Sasa swali linalofuata chini ya hilo ni...Upesi sasa ili tulipate.

**88. Kuna tofauti gani kati ya mwili, nafsi, na roho?**

172 Mwili ni nyama unazozitazama na hauna budi kuoza. Ulizaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili za baba na mama. Lazima uoze. Si mzuri. Kwa hivyo katika kuzaliwa mara ya pili, katika ufufuo wakati—wakati utakapofufuka tena katika mwili mpya, ile nguvu ya uumbaji ya Mungu ndiyo itakayonena kama vile Yeye alivyofanya kwa Adamu kisha utafufuka.

**89. Tafadhali eleza nadharia yako kuwa Hawa alidungwa mimba ya Kaini na shetani?**

173 Sikusema hivyo kamwe; nilisema Hawa alipata mimba ya Kaini kutoka kwa nyoka. Katika Mwanzo 4, mara moja—kifungu cha 1, chaeleza dhahiri kuwa Adamu alimjua mke wake; naye

akapata mimba, na akamzaa Kaini, na kusema, “Nimempata mtoto mwanamume kwa Mungu.” Bila shaka! Uhai wote yabidi uje toka kwa Mungu. John Dillinger alitoka kwa Mungu. Adolf Hitler alitoka kwa Mungu. Kila . . . George—George Whitefield alitoka kwa Mungu, na hata Bob Ingersol. Kila mtu alitoka kwa Mungu.

174 Lakini nililosema ni hili. Nami nataka mtu fulani alibomoe. Ona? Biblia ilisema kuwa Yeye angeweka (katika Mwanzo 3:8). Ni . . . Lile . . . Swali lile lilipoulizwa wakati Hawa alikuwa amekuwa—kitu fulani kilikuwa kimetendeka kwake, yeye alikutana na huyo nyoka . . . Sasa yule nyoka hakuwa nyoka; yeye alikuwa mnyama, mjanja sana kuliko kila kitu makondeni. Hakukuwa na cho chote . . .

175 Siku hizi sayansi inatafuta mfupa wa mnyama fulani unaounganisha mwanadamu na nyani pamoja. Ulio karibu sana wanaoufikia ni wa sokwe. Hawawezi kupata mfupa wo wote. Hawataweza, kwa sababu ni nyoka. Ni ufunuo wa Mungu.

176 Tazama! Nyoka alikuwa ka—kama mtu wa zamani, kabla ya kuandikwa historia, kitu fulani cha pili kutoka kwa Mungu—ama kutoka kwa mwanadamu. Na hilo ndilo jambo pekee. Kama mnyama mwingine awaye yote ange—Shetani angeliwaingia, mbegu haingechanganyikana na za mwanamke. Huwezi kuchanganya mbegu za binadamu na mbegu za mnyama wo wote. Haiwezekani. Lakini mnyama huyu atakayechanganyisha mbegu ame—hayupo tena. Mungu alimgeuza kuwa nyoka. Lakini kumbuka wakati . . .

Kasema, “Mbona ulijificha? Mbona ukajifunika mwenyewe kwa majani ya mtini?”

Ndipo wakaanza kulaumiana kama ilivyo jeshini. “Vema,” Adamu akasema, “mwanamke uliyenipa alinishawishi kula hilo tunda.”

177 Basi mwanamke huyo akasema, “Nyoka alinidanganya.” Sasa, *kudanganya* maana yake nini? “Yeye—yeye alinidanganya.”

178 Kisha Mungu akasema, “Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka.” Uzao! Nyoka alikuwa na uzao halisi, na ulipitia kwa Kaini. Kupitia kwa Kaini wakaja watu wote werevu, watu walioelimika, hata siku zile zilizotangulia gharika. Na hatimaye akaja Habili aliyeuawa, na Sethi akainuliwa mahali pake kuonyesha kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu. Na toka kwake kukaja watu wanyenyekevu, wachungaji na kadhalika, lakini watu wamchao Mungu. Na Yesu alisema wana wa ulimwengu huu wana akili, ni werevu, kuliko wana wa Ufalme. Hiyo ni kweli!

179 Hatuwezi kulinganishwa nao. Usijaribu kujiinua juu upate kuwa kama wao. Jinyenyekeze mbele za Mungu. Usitamani kuwa mwenye akili na mwerevu. Tamani tu kumjua Yesu tu,

kwa maana huko ndiko kwenye uzao wa nyoka siku hizi. Na watu wanajidai kwa sababu wanasayansi, na watu werevu, na walioelimika, na wanavyuoni mashuhuri ni washiriki wa makanisa yao. Heri niwe na mtu aliyemjua Mungu hakika ijapokuwa hakujua a-b-c zake awe mshiriki wa kanisa langu (vema!) mradi awe ni mzao wa Kristo.

180 Mzao wa mwanamke, yule Mzao wa mwanamke alikuwa Kristo. Mariamu alimzaa Kristo. Na ule uzao wa nyoka uliokuwa Kaini uliendelea hata ukamfikia Yuda Iskariote. Walikuwako wote wawili Yesu na Yuda waliofanyika mwili papo hapo, Mungu na shetani. Kule msalabani Kalvari kulikuwako watu wanne wakifa. Kulikuwako mwivi kila upande wa Yesu, na Yuda akajinyonga mwenyewe kwenye mkuyu, ambao ni msalaba: "Alaaniwe aangikwaye juu ya mti."

Pale mwizi mmoja alisema, "*Ikiwa* wewe u Mwana wa Mungu, tushushe chini sisi."

181 Mwingine akasema, "Bwana, tunapokea haki yetu, tunaadhibiwa; Wewe hujatenda lo lote. Nikumbuke utakapoingia katika Ufalme Wako."

Yesu akasema, "Hivi leo utakuwa pamoja nami peponi."

182 Ndiye huyo—huyo Yesu, mhubiri Injili, akihubiri msalabani. Ndiye huyo Shetani akirudi kuzimuni, akienda zake pamoja na mzao wa nyoka, asiyeamini. Ndiye huyo Mungu akirudi Mbinguni pamoja na mwenye dhambi aliyetubu, yule mzao wa mwanamke. Bila shaka!

183 Haikuwa mzao wa shetani; ilikuwa mzao wa nyoka. Naye nyoka alikuwa na mzao; Biblia ilisema alikuwa na mzao. Na bado ungaliko leo, ule uzao wa nyoka. Mambo mengi . . .

Sasa, unaweza kuniuliza swali lingine juu ya hilo. Kama tungekuwa tu na wakati, nina maneno yote kwa ajili yenu, na . . .

**90. Tafadhali eleza maana ya "hatendi dhambi" katika 1 Yohana 5:18?**

Lo, tumelifika, naamini hapa. Labda . . . Nimelipata; nimelifungua moja kwa moja. Labda Bwana alitaka nilisome. Vema, 1 Yohana,

> *Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; . . .*

184 Hakika hatendi! Nimekwisha eleza hilo. Yeye hawezi kutenda amezaliwa na Mungu. "Hatendi dhambi" yeye hawezi kutenda dhambi, mbegu hiyo inadumu ndani yake. Andiko lingine ambalo huenda ukalitaja hapa lingekuwa Warumi 4:8, 4 na 5-8 ambapo Mungu . . . Daudi alinena, samahani miaka mingi iliyopita na kusema, "Heri mtu ambaye Mungu hatamhesabia dhambi (ona?) kwa sababu yeye hatendi dhambi."

Sasa, tunalo moja zaidi ndiposa tumalize. Hebu tuone!

**91. Ndugu Bill, nini tofauti kati ya uasherati na uzinzi, Mathayo 19:9?**

185 Yesu alisema katika Mathayo 19:8, "Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini." Tofauti kati ya uasherati na kuzini, maneno hayo yangetumiwa kwa njia zote mbili. Lakini kuyafanya dhahiri yale Yeye alikuwa akinena pale, kuwa mwa—mwanamke ambaye hajaolewa hawezi kuzini, kwa sababu yeye hana mume wa kuzini dhidi yake. Ni unajisi kwake. Yambidi aungame hilo kwa mumewe kabla hawajaoana kama yeye alitenda hilo. La sivyo, na mumewe agundue hilo baadaye, yeye ana haki ya kumtaliki, kwa sababu yeye aliweka nadhiri ya uongo. Kwa maana Biblia ilisema—"Na iwe vema . . . " au kawaida za dini zasema, "Na ijulikane vema kwenu (ninayo kwa yangu) ya kwamba kama mume na mke wo wote wakiunganishwa vingine isipokuwa vile Neno la Mungu linavyoruhusu, ndoa yao si halali. Nitahitaji na nitawaagiza ninyi nyote wawili kwa kuwa bila shaka mtahukumiwa katika ile siku ya hukumu wakati siri zote za mioyoni zitakapofichuliwa, kama mmoja wenu anajua kizuizi cho chote kwa nini msifunganishwe pamoja kihalali, na aungame sasa." Naam. Ona?

186 Kwa hivyo uasherati ni wakati msichana, anapoishi kichafu, huo ni uasherati, kwa sababu hana mume. Lakini anapoolewa, ndiposa anaishi hivyo, anazini dhidi ya memewe.

187 Mwanamke fulani alikuja wakati mfupi uliopita, naye akasema, "Ee, nimeungama hayo yote." Alikuwa na wasiwasi, alikuwa na ugonjwa wa akili, kisha kusema, "Nimeungama hayo yote kwa Mungu."

188 Nikasema, "Inakubudi uyaungame kwa mumeo. Hukuzini dhidi ya Mungu; ilikuwa mumeo." Hiyo ni kweli.

189 Na mwanamume akimwoa mwanamke naye ameishi kinajisi kabla hajaolewa, kisha aje kwake, haidhuru wameoana kwa muda mrefu vipi, ndiposa mwanamke huyo amjie na kusema, "Mpenzi, nataka kukwambia jambo fulani. Nilienda na mwanamume mwingine, sikukwambia kamwe," Yesu alisema ana haki ya kumtaliki na kuoa mwingine, kwa sababu hawajaoana tangu mwanzo, kwa sababu yeye alimwambia uongo aka—akamdanganya.

Sasa, kuna jambo lingine hapa . . . Asante.

**92. Tafadhali fafanua 1 Yohana 5:16**

I Yohana 5, tunayo papa hapa.

*Mtu akimwona ndugu yake anatenda dhambi isiyo ya mauti, ataomba, na Mungu atampa uzima kwa ajili ya hao watendao dhambi isiyo ya mauti. Iko dhambi iliyo*

*ya mauti. Sisemi ya kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo dhambi.*

190 Vema, Twende. . .Hebu turudi nyuma upesi na tulipate, hili ni la mwisho. Hebu tufungue Marko, na hili litaeleza tu hasa dhambi iliyo ya mauti ni gani. Kuna dhambi iliyo ya mauti, na hata usiombee dhambi hiyo. Wangapi wanajua kuwa kuna dhambi iliyo ya mauti. Hata huiombei. Chukua Marko, sura ya 3 Marko. Na baada ya kupata sura ya 3 ya Marko, ndipo upesi tutachukua hili Andiko moja kabla hatujafunga. Hebu tuende kwa 3 na 22.

*Nao waandishi walioshuka kutoka Yerusalemu wakasema, Ana Beelzebuli,*. . .(walimwona Yeye akitambua mawazo ya watu.). . .*wakasema, Ana Beelzebuli, na, kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo.*

*Akawaita, akawaambia mfa—mfano, Awezaje Shetani kumtoa Shetani?*. . .(sasa, kama shetani aweza kuponya, awezaje?) *Awezaje Shetani kumtoa Shetani?*

*. . .ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, ufalme huo hauwezi kusimama.*

*Na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama.*

*Na kama Mimi—Na kama Shetani ameondoka juu ya nafsi yake, akafitinika, hawezi kusimama, bali kuwa na kikomo.*

*Hawezi mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu; na kuviteka vitu vyake, asipomfunga huyo kwanza yule—mwenye nguvu ndipo atakapoiteka nyumba yake.*

Awezaje kuingia ndani mle, katika mioyo hiyo na apate kile. . .(Ona?) isipokuwa ni ya Mungu?

*Amini, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa. . . wanadamu, na kufuru zao watakazo. . .wao zo zote—watakazokufuru zote;*

*Bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele, ila atakuwa ana dhambi ya milele;* (Huo ni utengano!)

*Kwa vile*. . .(Mbona Yeye alisema hayo?). . .*Kwa vile walivyosema, Ana pepo mchafu.*

191 Kuita Roho wa Mungu aliyekuwa akitenda miujiza hii katika Kristo, walisema alikuwa ni Roho wa shetani anayetenda hayo; Yesu alisema ni dhambi isiyosamehewa. Na ukimwona mtu. . .Omba—usimwombee kama yeye anamfanyia mzaha Roho Mtakatifu na kunena dhidi ya Roho Mtakatifu, umekatazwa hata kumwombea mtu kama huyo. Wafahamu hilo? Kwa maana kuna dhambi iliyo ya mauti. Kunayo dhambi moja pekee. Yesu

alisema aina zote za dhambi watasamehewa wanadamu, lakini kumkufuru Roho Mtakatifu hakutasamehewa.

192 Sasa watu husema, "Vema, kumkufuru Roho Mtakatifu, . . . " *kukufuru* ni nini? Maana yake ni "kunena, kudhihaki, kufanyia mzaha, kutukana." Vema!

193 Walimkufuru Yeye vipi? Kusema kuwa yule Roho Mtakatifu aliyekuwa ndani Yake, akimfanya atende na kufanya mambo ambayo Yeye alikuwa akitenda, wao walisema, "Yeye amepagawa na Beelzebuli, shetani. Na hiyo maana yake ni shetani, mpiga ramli ndani Yake akimfanya kutenda mambo hayo. Kuona siri katika mioyo ya watu, na kumwambia Filipo Yeye alijua alipokuwa kabla hajaja mkutanoni, na kutoa pepo, na kufanya mambo hayo pale, Yeye anayafanya kwa Beelzebuli, na Yeye ni Shetani." Na Yesu alisema dhambi hiyo haitasamehewa kamwe, kwa hivyo hiyo ni dhambi isiyosamehewa ambayo haipaswi kamwe kuombewa. Haitasamehewa kamwe. Mwanamume na mwanamke afanyaye hilo amejiondolea mbali na Uwepo wa Mungu milele na milele, hamna msamaha.

Je, mwampenda?

Nampenda, Nampenda
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

194 Sikizeni, mmekuwa wazuri sana, na huu umekuwa mzito, na umechukua muda mrefu. Sasa mmeketi kanisani humu tangu saa moja u nusu, saa mbili u nusu, saa tatu u nusu, masaa mawili na nusu, mkiketi humu katika kanisa lenye joto. Hamkufanya hivyo mketi tu humo. Nami nafikiri asilimia tisini na nane au tisini na tisa ya makutano wameketi vitini mwao tangu wakati huo. Nataka kusema hili: Jeffersonville, najisikia hivi: kuwa umetenda dhambi ukamaliza siku zake za neema . . . Naamini hilo. Naamini nchi nzima ya Marekani imefanya hivyo, lakini nina baadhi ya marafiki waaminifu zaidi ulimwenguni papa hapa Jeffersonville. Nina watu hapa ambao wangalinifia.

195 Sasa, usiku kama huu wenye joto, wageni walio malangoni mwetu, niambie ambapo mtu angeketi tu kumsikia mtu mwingine, labda akiongea juu ya Maandiko ambayo hata hawaamini jinsi ningeyaeleza, lakini ni wanyenyekevu na wacha Mungu kutosha kuketi na kusikiza. Na mkaishi maisha marefu. Nyota zirudipo mavumbini, na mwendelee kuishi katika Kristo Yesu. Na Mungu awajazie kila kitu mnachohitaji. Na awape haja za mioyo yenu. Kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi Wake na kuamini kuwa maombi yangu yangewasaidia, na Mungu wa Mbinguni aliyemfufua Mwanawe, Yesu Kristo, kuwa patanisho la dhambi zetu, kufa badala yenu, na Yeye aliye na nguvu zote, Yeye yule aliye kila mahali hapa katika jengo hili sasa, na

awape haja ya mioyo yenu ndilo ombi langu nyenyekevu kwa kila mmoja wenu. Na katika nchi ambayo jua halitawaka juu yenu tena kuwachoma, ambamo upepo wenye joto hautavuma, natumainia kuwa na miaka milioni ya miaka nitakapoketi na kila mmoja wenu katika Ufalme wa Mungu na kuongea kuhusu vitu vya milele vya usiku huu mwingi na kadhalika jinsi tulivyoketi pamoja. Nakusudia hayo na yote yaliyo ndani yangu, moyo wangu wote. Naomba kuwa Mungu atawapa ninyi hayo kila mmoja wenu.

196 Neema Yake na iwe pamoja nanyi. Yeye na awaponye magonjwa yenu. Yeye na awape ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nami nasema hili sasa bila hata . . . Kama nilikwaza kwa lo lote nililosema kuhusu uzao wa nyoka, ubatizo katika Jina la Yesu, ambapo mambo hayo . . .

197 Sasa mtu fulani asema, "Ndugu Branham ni wa umoja." La, bwana, mimi si wa umoja. Siamini kuwa Yesu angelikuwa baba Yake mwenyewe. Naamini kuwa Yesu alikuwa na Baba, na huyo alikuwa ni Mungu. Lakini Mungu aliishi na kuwa na maskani katika mwili huu unaoitwa Yesu, na Yeye alikuwa Imanueli, Mungu pamoja nasi. Na hamna Mungu mwingine isipokuwa Mungu huyu. Yeye ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Na Jina la, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu . . . *Baba*, Bwana, *Mwana*, Yesu, *Roho Mtakatifu*, Logos, Roho wa Mungu. Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, Bwana Yesu Kristo; ndiye Huyo. Na ndani Yake mlikaa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili.

198 Nami naamini bila shaka yo yote, nikiwapenda ninyi, na haidhuru kama mtabaki mmebatizwa kwa Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, mmenyunyuziwa, mmemwagiwa, cho chote mtakacho, naomba Mungu kwa nafsi yangu yote na mwili wangu wote kuwa ninyi na mimi tutakutana katika Ufalme wa Mungu, na Mungu atasahau, kama nimekosea, atasahau yangu, kama umekosea atasahau yako. Lakini katika—kwa kuamini kwangu mwenyewe kwa Maandiko nikijaribu kulenga shabaha toka Mwanzo hadi Ufunuo, nawaamuru ninyi mbatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo kama hamjabatizwa hivyo.

199 Na kama hujampokea Roho Mtakatifu, na maisha yako si mema, haijalishi kama ulinena kwa lugha, kama umepiga shangwe, kama umeruka juu-chini, kama umeweka mikono juu ya wagonjwa nao wakapata afya, kama umetenda namna zote za miujiza na ishara, kama hujapata matunda ya Roho, upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, upole, saburi, imani na mambo haya yote ndani yako, ndipo nawaamuru na kuwashurutisha ninyi kwa Jina la Yesu Kristo, msikome kuomba hadi Roho Mtakatifu awashukie! Haidhuru umenena kwa lugha mara ngapi, umepiga shangwe mara ngapi, umekuwa mshiriki wa kanisa mara ngapi, kama umekwisha kuwa hapa, yale yote umekwisha tenda hayatafaa kitu hadi Kristo, Roho Mtakatifu,

achukue nafsi moyoni mwako na umekufa kwa mambo ya dunia na unaishi upya katika Kristo.

200 Mungu awabariki ndilo ombi langu. Hebu tusimame kwa miguu yetu. Jamani, hili ni kusanyiko nzuri. Mmekuwa wazuri sana; nachukia kuwaacha mkisimama hivi.

Maskini Edith kule nyuma ana maulidi. Edith, naweza kuhesabu. . . Nitamwamuru Ndugu Neville akuwekee wewe hivi. Tutaona huyu msichana ana umri gani. Umri wa miaka thelathini na minane. Mungu akubariki. David, tupe—samahani, ni Teddy, tupe sauti ndogo, *Maulidi Njema Kwako*, vema ukiweza.

Maulidi njema kwako;
Maulidi njema kwako;
Maulidi njema, Dada Edith;
Maulidi njema kwako.

Sasa, kusanyiko hili lote tuimbe pamoja, *Hatutazeeka Kamwe*. Haya, nyote pamoja sasa.

Hatutazeeka kamwe, hatutazeeka kamwe,
Katika nchi ambamo hatutazeeka kamwe;
Hatutazeeka kamwe, Hatutazeeka kamwe,
Katika nchi ambamo hatutazeeka kamwe.

Twonane milele,
Twonane bandarini kule.
Twaonane milele,
Twaonane bandarini kule.

*Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa*, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org